# *Isikie Sauti Yake*

Asante, Ndugu Neville. Naamini ilisemwa na Daudi, "Nilifurahi waliponiambia, twende nyumbani kwa Bwana." Kuna kitu fulani kuhusu shule ya Jumapili ambacho sehemu zingine za ibada hazina, wakati mwingine wowote siku nzima. Tumeamka hivi punde kutoka kwa mapumziko ya usiku mwema, na—nasi tunajisikia tu tofauti, nawe umechangamka na uko tayari kwa siku hiyo.

2 Sasa tunaelewa kwamba...Jana usiku, tuliwauliza wa—watu kama walikuwa na kanisa lao...ambalo walikuwa wakihudhuria, wakati wakitembelea au—au...ninamaanisha, washiriki wa kawaida wa makanisa, kwamba wanapaswa kuhudhuria kanisa lao wenyewe asubuhi ya leo. Maana, sisi tukiwa wa madhehebu mbalimbali, hatupendi kabisa kuwachukua watu kutoka katika kusanyiko lao wenyewe.

3 Nami nimeshutumiwa mara nyingi juu ya—ya kuyahukumu makanisa mengine. Hiyo si kweli. Siyahukumu makanisa mengine. Ninalaumu, mara nyingi, mambo ambayo—ambayo wanayaridhia, bali bila shaka silihukumu kanisa. Lakini, mara nyingi, wanapofundisha mambo ambayo ni kinyume na Maandiko, basi ni—ninahukumu hilo. Na halafu wanapofanya mambo ambayo ni dhambi, na—na kuyaruhusu makanisani mwao, ninahukumu hilo. Lakini kamwe...Kama tu isemwavyo...Nina marafiki wengi Wakatoliki wanaoketi hapa, wala kamwe siwahukumu Wakatoliki. Ninahukumu fundisho la kanisa Katoliki, maana siamini ni la Kimaandiko. Wala si zaidi ya vile ninavyoyahukumu mengi ya madhehebu ya Kiprotestanti, maana sidhani ni ya Kimaandiko. Nami ninawajibika kuitetea Kweli. Mnaona? Unajua, Mungu atakuthamini ikiwa utakuwa mwaminifu, mkweli tu.

4 Unajua, mara nyingi, mwanamume anayetafuta mke, mwanamume halisi ambaye ana uanaume nyuma yake, kwa jumla hatafuti msichana aliye m—mrembo sana usoni, ama kadhalika. Anajua huo utatoweka, moja ya siku hizi. Mnaona? Anamtafuta mwanamke ambaye ni mwanamke katika utu, mwanamke halisi. Na ikiwa yeye ni mwaminifu, na ni mwanamke halisi, mwanamume huyo atamthamini. Sijali yeye ni jamaa m—mbaya jinsi gani, na jinsi anavyozurura na—na wanawake wabaya; hakuna mwanamume mbaya duniani asiyeweza kumthamini mwanamke ambaye atatetea jinsi mwanamke apaswavyo kuwa. Hiyo ni kweli. Kwa sababu, anathamini hilo.

5 Na hivyo ndivyo ilivyo kwa—kwa kulihubiri Neno, endapo mtu atasimamia tu yale anayoamini. Sasa si...Kumbuka,

Mungu anaujua moyo wako. Na kama utasimama na kile unachoamini kabisa kuwa ni Kweli, basi unaweza kuwa na imani katika kile unachozungumzia.

6 Nina baadhi ya marafiki wazuri hapa. Ndugu Charlie Cox, namwona ameketi pale nje. Na majuma machache yaliyopita, nimekuwa huko Kentucky pamoja naye, tukiwinda kuchakulo, ambako nilipumzika kidogo. Ndugu Banks Wood. Na, sasa, sisi, tunafanyiza bunduki zetu mazoezi, wao . . . Sina budi kuifanya yangu kamilifu sana hivi kwamba italenga shabaha yadi hamsini, la sivyo si—siwezi kuwinda. Mnaona? Hivyo tu.

7 Vema, kuna faida gani kulenga shabaha? Mnaona? Kwa sababu, iwapo unampiga kuchakulo risasi, na kumpiga risasi kichwani, na kichwa chake labda ni kikubwa *hivyo* kote, popote chini ya inchi moja itakuwa ni sawa, mnaona, popote pale. Yeyote wa wavulana hao anasema, "Hiyo ni sawa. Nilimpiga kuchakulo." Wanaenda na kumwokota huyo kuchakulo. Lakini, kwangu mimi, haina budi kuwa kamilifu kabisa. Haina budi kupiga shabaha yenyewe. Haiwezi kukosea kwa robo inchi. Lazima ipige penye hiyo shabaha, la sivyo ninashikwa na wasiwasi na fadhaa kabisa.

8 Nami nilikuwa nimeketi chini, hivi majuzi, msituni, nami nilikuwa nikisema, "Bwana, mbona—mbona nishikwe na kichaa hivi? Kwa nini ulinifanya kichaa hivi?" Nikasema, "Sasa hapo . . . "

9 Ndugu Banks alikwenda kuwinda na bunduki yake, naye akaivuta ili kutupa risasi, ikiwa na darubini. Na wewe tu . . . Kila mara baada ya muda fulani, ungeninii . . . moja itafyatuka, maana ikiwa . . . Risasi zilizopakiwa kiwandani zitafanya hivyo, kwa vyovyote vile, maana una baruti nyingi kidogo, na baruti kidogo zaidi. Lakini ingepiga kando kidogo tu, ama inchi moja ama mbili, Ndugu Banks aseme, "Loo, hiyo ni sawa, nilimpiga risasi kuchakulo. Hiyo ni sawa." Hali—halimsumbui. Charlie, vivyo hivyo. Lakini mimi . . .

10 Yangu haina budi kupiga shabaha, papo hapo katikati, la sivyo inaniudhi. Nikasema, "Nimekuwa kichaa wa kawaida." Ndipo basi nikaanza kuangalia nyuma, nami nikaona kwamba maisha yangu yako hivyo. Hayo ndiyo maumbile yangu. Basi nikawazia, "Vema, mbona ukaniumba hivyo?" Hata inanifanya kushikwa na wasiwasi kama—kama ikikosea kidogo tu upande *huo* au upande *ule*. Na hivyo ndivyo Bwana alivyonifunulia, nikiwa nimeketi chini pale, kwenye Kibonde cha Mlafi, popote tulipokuwa, tukiwinda. Hapo, naamini panaitwa Dutton; lakini, kuchakulo wanakula haraka sana, ninapaita, "Mlafi." Kwa hiyo wao . . .

11 Juu ya mahali hapa, niliwazia, "Ndivyo hivyo." Nisingeweza hata kufundisha kwamba kulikuwako na kuzimu mpaka nilipokuwa na uhakika wake. Mnaona? Na kwa hiyo kama

Maandiko yanatabiri uponyaji wa Kiungu, na *hapa*, inaonekana *hivi* na *vile*; kama Maandiko yanasema, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," kana kwamba kuna Miungu watatu, na *Hapo* naona kuna Mmoja tu; na sasa nitafanyaje shaghalabaghala, kuhusu watu wengine, kile wanachosema juu Yake, nilichukue hivyo? Kama Biblia inazungumza juu ya kuchaguliwa tangu zamani na neema, na *hapa* ina matendo, na *hapa* ina neema. Basi si—siwezi kuihubiri hivyo.

12 Sina budi kutatua hilo, na kote, na kote, na kote katika Biblia, mpaka ilenge shabaha kikamilifu, mnaona, mpaka itokee kikamilifu katika Maandiko. Ndipo ninaposimama, ninaweza kweli kuwa na imani katika kile ninachofanya, mnaona, kujua ya kwamba unachohubiri ni Kweli. Unaona? Na basi kama mtu yeyote akilipinga Hilo, tayari umesoma vya kutosha mpaka unajua hasa Yeye anasema nini, mahali pa kumsimamishia, unaona, papa *Hapa*. Unaona? Na hivyo ndivyo ilivyo. Mungu hutufanya kwa njia tofauti, hata kwa urahisi tunaweza tu... Hiyo inafanya ulimwengu kuwa hivyo. Lakini, hilo ndilo linalonifanya kushikwa na wasiwasi, mtu mwenye fadhaa. Halina budi kuwa sawa tu.

13 Nami nina furaha sana, usiku wa leo, leo hii, asubuhi ya—ya leo, kusema kwamba ninajua ya kwamba Bwana Yesu hajafa. Yu hai, na yuko papa hapa sasa kama alivyokuwa wakati wowote ulimwenguni kule Galilaya ama popote pale. Yeye ni Mwana wa Mungu aliye hai, aishiye, aliyefufuka, aliye kila mahali. Hiyo ni... Na kama nisingeweza...

14 Kama nilifundisha Maandiko ya Mungu fulani wa kihistoria, wala sikuwa na hakika ya kwamba alikuwa papa hapa, ni—ningechanganyikiwa kabisa. Ingenitia wasiwasi sana, nisingejua nilichokuwa nikifanya. Mnaona? Wala nisingejua mahali pa kuwaambilia watu, "Vema, sasa, Yeye atafanya *hivi*, ama atafanya *vile*." Ni—nisingeweza kuwaambia. Sijui. Lakini ukijua alichoahidi atafanya, na umemwona akikifanya, basi unajua unaposimama. Unaona? Na kuona jinsi Mungu, katika mipango Yake mikuu, alivyojua tu jinsi ya kumfanya kila mtu kuwa kitu fulani hasa, maana Yeye atawatumia kwa kusudi hilo.

15 Mlimsikia maskini mama huyo hapa juu, muda mfupi uliopita? Bibi Stricker, akiimba bila muziki wowote. Alikuwa na namna fulani ya kitu kidogo alichokuwa akipulizia, kupata tuni yake, sauti ya—yake au chochote mnachokiita. Naye angeweza kusimama na kuimba kwa sauti hiyo ya chini kabisa, na kuiinua juu, ule, *Meli Hoyee!* Sasa, mnapaswa kunisikia nikiujaribu huo wakati mmoja. Ungekuwa mbaya sana. Lakini, mnaona, Mungu alijua jinsi tu ya kumfanya mwanamke huyo apate kufanya hivyo.

16 Na hiyo ndiyo njia. Sisi sote tuna maumbile tofauti. Laiti tungelipata tu nafasi yetu katika Kristo, na hapo tukae na kumtumikia.

17 Namwona maskini msichana mdogo ameketi hapa, asubuhi ya leo, kwenye kiti cha magurudumu. Nakutakia heri. Ni kitu gani kilichokulemaza, kipenzi? Ninii ya misuli . . . udha- . . . Loo, siwezi kutamka neno hilo, ninapoanza; udhaifu wa misuli, au chochote kile. Je, ndivyo ilivyo, kipenzi, kilichokulemaza, au ni polio? Polio. Unajua, Yesu huwaponya wasichana wadogo. Sivyo? Wewe ni msichana mdogo mrembo sana. Nami ninaamini Yesu atakujalia kupona.

18 Jana usiku, wale wasichana wawili wadogo waliokuwa wameketi hapa na ugonjwa huo ambao hakuna hata mtu mmoja duniani ajuaye ni nini. Vidole vyao vidogo vinaanguka, na miguu yao midogo ikaanguka. Wasichana wawili wadogo warembo. Na inatokea ninamfahamu mama yao na bibi yao. Nami nikajisikia tu kuongozwa kumhukumu huyo ibilisi ambaye angewatesa hao watoto wadogo walioketi pale; moja kwa moja. Nao wamekuwa kwenye viti vya magurudumu kwa sijui muda gani. Ndipo jana usiku, habari zikaingia ghafla, mstarini, "Wale wasichana wadogo wamesimama, wanatembea huku na huku." Unaona hilo, kwamba—kwamba Bwana Mungu aliwarehemu sana. Loo, Yeye ni mwema sana kwetu! Tunapaswa kumthamini zaidi.

19 Basi nilikuwa nikiwazia, jana usiku tu, nikiisha kwenda nyumbani na kujilaza kitandani kwa dakika chache, nilikuwa nikifikiria juu ya, "Nafsi inapotoka ndani ya mtu, kuna nini?" Ni utu wake wa ndani ambao umetoka. Hajafa. A—angali hai. Mnaona? A—anaishi milele. Nao wapendwa wetu ambao wamepita ng'ambo ya pazia hili, wako katika mwi—mwili ambao hatujui ni nini. Haujafunuliwa.

20 Kuna hatua tatu za kila kitu. Kuna hatua ya mwili unaopatikana na mauti, mwili usiopatikana na mauti, na halafu mwili uliotukuzwa. Mnaona? Kama tu vitu vingine, kama vile . . . Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, huingia mkondo mmoja, na hao watatu hufanya Mmoja. Kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, katika mkondo, humfanya mtu huyo. Kisha, na nafsi, mwili, na roho, hufanya mmoja. Nao husafiri tatu-tatu, na tatu ni moja. Basi chukua ki—kipande cha kioo chenye ncha tatu kisha ukiweke juani, kitaakisi rangi, hata hivyo, rangi saba zitaishia kwa moja.

21 Na ukichukua nyekundu, na kuangalia kupitia nyekundu kwenye nyekundu. Ni wangapi wanaojua itakuwa rangi gani? [Kusanyiko linasema, "Nyeupe."—Mh.] Nyeupe. Uh-huh. Si ajabu hiyo? Kwamba, nyekundu kupitia nyekundu, inaonekana nyeupe. Nyekundu ni ishara ya ukombozi. Ndipo wakati wewe . . . Mungu anapotazama dhambi zetu nyekundu, kupitia Damu nyekundu ya Mwanawe wa thamani, ni nyeupe. Kwa hiyo, lakini, Yeye hana budi kuangalia kupitia kwenye ile Damu. La sivyo, wao ni wenye dhambi. Kwa hiyo hatuna budi kuwa chini ya Damu.

22 Basi nafsi inapouacha mwili, husafiri kwenda mahali pake pa kupumzikia, katika mwili ulio katika umbo na sura ya mwili huu, ila si mwili wa aina hii. Utakutana na wapendwa wako. Usingeweza kuwasalimia kwa mkono. Ungeweza kuzungumza nao, ungeweza kuwaangalia. Wanaonekana kama tu wanavyoonekana hapa. Maana, wakati Petro, na Yohana, na Yakobo, walipomwona Musa na Eliya, waliwatambua, kwenye Mlima wa Kugeuka sura. Lakini, ni mwili.

23 Lakini basi wakati mwili huo, kwa namna fulani mwili wa kimbinguni, unaporudi duniani, unachukua du—dutu ambayo hapo awali uliishi ndani yake, na kisha unakuwa mwili uliotukuka. Na mwili huo ndio tutakaomwonea Bwana Yesu, katika mwili Wake uliofufuka. "Bado haijaonekana tutakavyokuwa," alisema Paulo, "lakini tunajua tutakuwa na mwili kama mwili Wake Mwenyewe wa utukufu, kwa kuwa tutamwona jinsi alivyo."

24 Nayo mikono hii yote ya kale yenye makunyanzi na tishu zilizovunjika zote zitafifia zikawa fahari ya ujana. Enyi wanaume na wanawake wazee, kumbukeni, ninyi . . . Hii ni . . . Hiyo, hiyo ni alama ya kule kuanguka, uzee wenu. Lakini katika ufufuo, hawatakuwa na alama moja ya chochote cha dhambi. Lakini kwa nini Mungu alikuumba jinsi alivyokuumba? Alikufikisha kwenye umri fulani, ulipokuwa na umri wa yapata miaka ishirini na miwili, ishirini na mitatu, ulikuwa katika upeo wako. Ulikuwa ukila chakula na kupata nguvu zaidi, na afya njema, na jinsi ulivyoonekana mtu mwenye nguvu. Halafu, baada ya hayo, ukaanza kupata makunyanzi, unaona, mauti ikaingia. Lakini, katika ufufuo, uzee wote utafutiliwa mbali.

25 Ninamwangalia hapa maskini mhubiri mmoja mzee na mkewe. Wako katika umri wa miaka themanini na kitu, nadhani. Ndugu na Dada Kidd, wakiihubiri Injili labda kabla sijazaliwa; nami ni mzee. Nami ninawaona wameketi hapa, maskini mume na mke, wenye nyuso za amani. Nami nawazia tu, ya kwamba, katika ufufuo, watakavyoonekana. Hayo makunyanzi ya kale, na mikono inayotetemeka na kupooza, na mvi zitafifia zikawa fahari ya ujana. Ina faida kweli kumtumikia Bwana. Ina faida kweli. Tutamwona, siku moja.

26 Sijui kama Rosella Griffin yupo. Ningependa kumfanya aseme neno. Maskini mlevi sugu aliyeponywa hivi punde huko . . . hapa, miaka michache iliyopita. Na hiyo inaweza kumsaidia mlevi sugu aliye hapa. [Dada mmoja katika kusanyiko anasema, "Ndugu Branham, alienda nyumbani asubuhi ya leo."—Mh.] Ilimbidi kwenda nyumbani asubuhi ya leo. Sawa. Kisa cha ajabu! Nilifikiri jana usiku ilinipasa kumfanya aseme kitu. Ningemfanya, kama ningalijua, kwamba angeondoka asubuhi ya leo. Mambo mengi sana ninayotaka tu hawa jamaa wa maskanini wasikie.

27 Sasa, kuna yeyote hapa wa kubatizwa, asubuhi ya leo, majini? Hebu tuone. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, yapata sita ama saba hapa wa kubatizwa. Nayo ibada ya ubatizo itafuata somo hili la shule ya Jumapili.

28 Sasa, chumba cha shule ya Jumapili cha Dada yetu Arnold, cha watoto wake wadogo, kimekatiliwa mbali. Nasi tutaninii tu, mkipenda, Dada Arnold, karibu itatubidi kuiahirisha hiyo hadi kesho yake, kwa sababu hatuna nafasi kwa ajili ya hiyo shule. Nami nitasoma Maandiko fulani hapa katika dakika chache, kwa ajili ya watoto wadogo, na hilo litawapa kitu cha kuwazia, pia. Halafu basi Jumapili ijayo mtaendelea na ibada zenu za kawaida na shule ya Jumapili. Sasa, tunataka kusema . . .

29 Hili hapa jambo lingine ninalotaka kusema asubuhi ya leo. Ni—ni—niliwaambia wasifanye hivi, lakini wakafanya, kwa vyovyote vile. Mnaona? Hiyo ilikuwa, sadaka jana usiku iliyonijia, mnaona, sadaka. Niliwaambia wasifanye hivyo, mnaona. Nao . . . Lakini walifanya hivyo, kwa vyovyote vile. Na wakati . . . Sikujua mpaka Billy aliponiambia kwamba ndugu yangu Doc alikuwa amemletea, nyumbani kwake. Na sijazihesabu bado, lakini ninaamini kwamba iliripotiwa kwamba kulikuwa na karibu mia tatu, au zaidi kidogo ya mia tatu. Je, hiyo . . . Unakumbuka, Doc, zilikuwa ni ngapi? [Ndugu Edgar Branham anasema, " . . . ishirini na nne, kumi na mbili."—Mh.] Ati nini, ndugu? ["Tatu, ishirini na nne, kumi na mbili."] Mia tatu ishirini na nne, kumi na mbili. Nawashukuru, sana.

30 Sasa, nimekuwa sifanyi kazi kwa muda mrefu. Mnajua hilo. Na katibu wangu akiwapo, ama baadhi yao hapa asubuhi ya leo, wanajua ya kwamba matumizi yangu, haidhuru niko wapi, papa hapa nyumbani, hunigharimu zaidi ya dola mia moja kwa siku, kwa ofisi zangu na kadhalika kutuma leso na kadhalika ulimwenguni kote, katika matumizi.

31 Nami na—nataka kusema hivi, kuwatia moyo ninyi watu hapa, hata hivyo. Kwa idadi ya watu, hiyo ndiyo sadaka kubwa zaidi ambayo nimewahi kupokea maishani mwangu. Je, mnatambua kuwa hiyo inaweza kuwa karibu dola moja kwa kila mtu, wastani? Na karibu sadaka yoyote huko kazini kwa wastani itakuwa kama, yapata senti ishirini na mbili au ishirini na tano kwa kila mtu. Lakini hii ilikuwa dola moja kwa mtu kwa wastani. Maana, najua huwezi kuingia humu . . . Hawachukui sadaka huko nje. Wala hamwezi kusongamana katika mahali hapa padogo, yapata watu mia tatu, na—natilia shaka. Je, unajua maskani inakaa wangapi, Ndugu Neville? [Ndugu Neville anasema, "Inapaswa kuwa mahali fulani yapata mia tatu, jinsi ilivyo sasa."—Mh.] Takriban watu mia tatu. Kwa hiyo, mnaona, hiyo ni karibu do—dola moja kila mmoja. Mungu anajua jinsi ninavyothamini hilo. Nawashukuru sana. Nayo inaingia moja kwa moja katika kazi ya Bwana. Na—nawashukuru kwa ajili

yake. Na kwa . . . Kama baadhi yao wataondoka kabla ya usiku, maana . . . nami . . .

32 Niliporudi nyumbani jana usiku, kisanduku kidogo kilikuwa kimewekwa barazani, namna *hii*, na kilikuwa ni lu—lundo la jeli, ninaamini, hiyo inatoka kwa mtu fulani. Mnajua, napenda tu jeli. Na mimi—mimi ninathamini hilo. Na da—dada fulani hapa, ambaye afadhali nisilitaje jina lake. Yeye ni rafiki msiri wa familia yetu, naye aliacha zawadi ya upendo kwa mama yangu, kwa ajili yangu na kwa Billy. Hujui, dada, jinsi ninavyothamini jambo hilo, na jinsi ilivyokuja kwa wakati mzuri.

33 Na, loo, mambo mengi sana! Mnaelewa. Nami nina hakika ya kwamba Yeye anaelewa. Na kwa hiyo ninatumaini tu ya kwamba Yeye atambariki kila mmoja wenu, kwa wingi. Laiti ingewezekana niende nyumbani na kila mmoja wenu, na—na kukaa pamoja nanyi kwa muda kidogo, na kuzungumza nanyi. Ninapenda kufanya hivyo.

34 Lakini, ni, mnajua jinsi ilivyo, sikuzote inasonga mbele. Inabidi twende haraka. Kwa kweli, mara baada ya ibada usiku wa leo, Bwana akipenda, nitaondoka humu jimboni, mara tu ibada itakapofungwa. Sina budi kuondoka hapa kabla ya saa sita. Nina miadi ya saa sita. Nami nina ya kutosha, alasiri ya leo. Nami . . . Mnajua jinsi ilivyo. Ni kwenda tu mara kwa mara, wakati wote; watu ni wagonjwa, wanakufa.

35 Na mara nyingi ninaingia mahali fulani, na niwe tu nimesimama pale, ndipo mtu anaingia, anasema, "Unanijua, Ndugu Branham?"

"La, sikujui."

36 "Mbona, nilikuwa nimelala hospitalini, nikifa, ulipokuja ukaniombea. Bwana aliniponya." "Nilikuwa kipofu ulipokutana nami barabarani, siku hiyo ono likaja." Unaona? Na mimi—mimi kamwe sijui ni nini.

37 Lakini ninawazia wazo hili moja la baraka, Ndugu Egan, kwamba, siku moja wakati nimehubiri mahubiri yangu ya mwisho, nimemwombea mtu wa mwisho ambaye Bwana anataka nimwombee, kisha niende Nyumbani! Na katika asubuhi hiyo ya ufufuo, loo, itakuwa ni siku ya jinsi gani, furaha! Ninapoweza kusimama Pale, wakati malkia wa Kusini atakapokuja, ninaweza kuona ushawishi aliokuwa nao! Nitaona akija Kule, Billy Graham, ushawishi aliokuwa nao. Oral Roberts, na hao wengine wote, akina Sankey, Finney, Moody, Calvin, Knox, na kadhalika. Kisha nitaona kundi langu likija. Loo, hiyo itakuwa ni shangwe, huko kutakuwa ni kutiwa taji kwangu. Hiyo ni kweli. Na, kwa neema ya Mungu, natumaini kuwa na mamilioni kadhaa Huko.

38 Na sasa sina budi kwenda kwenye nchi za ng'ambo hivi karibuni. Na sasa, nijuavyo mimi, moja kwa moja katika mikutano yetu wenyewe, wazia tu jambo hilo, niko kwenye

milioni yangu ya pili ya nafsi, nikiwaleta kwa Kristo. Na—nami natumai kuwa nitawaona mamilioni mengi, mengi sana wakiletwa.

39 Sasa, ibada ya ubatizo, na sasa mi—miadi na kadhalika. Na, sasa, hii ni sikuzote baada ya mkutano.

40 Kama wakati wowote unarudi kwa ajili ya mahojiano ya faragha, ama kadhalika, mpigie simu tu wakala, Ndugu Mercier hapa. Inatubidi kuwa na namna fulani ya mpangilio, ambao inatubidi kuwa nao. Tunajua hilo. Naye Ndugu Mercier, huwaandikisha, anawaandikisha kadiri wanavyokuja, na mara miadi yangu ikiisha, yote ikiisha, mimi . . . Ninapoingia, ninampigia simu na kumwambia, "Nimemalizana na kundi hilo." Ananipa kundi jipya, nami huyo ninaondoka tena, mnaona. Basi, yote hufanya kutoka kwenye ofisi hiyo. Naye anajua tu jinsi ya kuyaweka ili aweze kumwingiza kila mmoja, awezaye kuingia, mnaona. Kwa hivyo, tuna furaha sana kuwa na ofisi hii ndogo inayofanya kazi jinsi ilivyo. Kwa hivyo hiyo ni BUtler 2-1519 tu. [Hiyo nambari ya simu imebadilishwa.—Mh.] Na hiyo ni . . . Au, ukipiga simu Jeffersonville, niite tu, nao watajibu hapo kwenye ofisi hiyo. Basi asanteni, sana sana.

41 Sasa hebu, kabla tu hatujafungua Neno Lake lililobarikiwa . . . Pia kumbukeni, mara baada ya ibada hii kwisha, na ibada ya ubatizo, Billy atakuwa hapa kusambaza kadi za maombi kwa ajili ya usiku wa leo.

42 Sasa, usiku wa leo ukiwa ni usiku wa kanisa, Jumapili usiku, karibu watu wote wa mjini watakuwa huko nje katika makanisa yao wenyewe, na karibu na Louisville na kote. Watakuwa katika makanisa yao wenyewe. Lakini wengi watakuwa tu ni watu wa nje. Kwa hiyo, nafikiri labda tunaweza kufanyiza mstari mkubwa wa maombi usiku wa leo na kumwombea kila mmoja wao. Ninatumaini kwamba tutaufanyiza. Tumesambaza kadi nyingi tu za maombi.

43 Na—nadhani, jana usiku, baada ya jana usiku, loo, nilijisikia tu kama ningechukua mojawapo ya hizo, loo, safari za ndege za peke yangu, mnajua, tunazozungumzia. Kuona tu, katika maskani hii ndogo ya kale, tena, mikono imeinuliwa juu.

44 Ninaye mvulana mdogo hapa, yeye ni mvulana kwelikweli, mtoto Joseph. Ana umri wa yapata miaka mitatu tu. Na wakati wote walipokuwa wakipiga kelele, kama hakuruka moja kwa moja pale katikati ya marefu ya kanisa na kutupa hiyo mikono juu, na kuanza kupaza sauti na kumsifu Bwana, moja kwa moja katikati ya marefu ya kanisa huko nje! Nami nafikiri, asubuhi ya leo, aligombana na dada yake mdogo, na kumuuma mkononi, kwa hivyo nikamwambia kwamba kupiga kelele kwake hakutakuwa na manufaa mengi mradi tu angefanya hivyo. Loo, jamani! Hao jamaa wadogo, wanaweza kukusumbua kweli, sivyo? Vema, bila shaka, jambo ni kwamba, aliwaona

tu wengine wote wakifanya hivyo naye akafikiria kwamba hilo ndilo alilopaswa kufanya, pia, na pengine kutufuata, jinsi tulivyokuwa tukifanya.

45 Sasa tuna Neno Lake limefunguliwa hapa. Sasa hebu tuzungumze Naye tu juu Yake. Sasa ninii tu . . .

46 Mungu Mpendwa, tunapokuja Kwako sasa hivi, kwa uchaji, kwa utulivu, kwa kiasi, na kwa imani, tukiamini ya kwamba Wewe unasikia na utajibu maombi. Kwa sababu, tunakuja katika hilo Jina litoshelezalo kwa yote la Mwanao, Bwana Yesu, ambaye Ndiye Yule asiyekosea, na akatoa ahadi, kwamba, "Mkimwomba Baba neno lolote kwa Jina Langu, nitalifanya." Ndipo tunajua ya kwamba tutapokea tu kile tuombacho, kwa maana tunakuja katika Jina Lake. Kwa maana hatuna Jina lingine ambalo tungeweza kukukaribia kwalo, Yehova Mungu mkuu, mwenye nguvu. Nasi tunakuja katika neema Yake, bila kukiri kwamba tunastahili chochote, bali kwa sababu Yeye ametufanyia upatanisho, kwa kuwa alitufia. Naye alilipia dhambi zetu, nasi tunajisikia ya kwamba tunaweza kusimama tukiwa tumehesabiwa haki machoni Pako, kwa kifo Chake. Hiyo ndiyo imani yetu. Wala hatuombi chochote ambacho kingekuwa kiovu, bali kile ambacho kingekuwa chema kwa kila mmoja wetu.

47 Kwa hiyo, Bwana Mungu, sema nasi kupitia Neno Lako. Na useme nasi katika Sauti hiyo, tupate kuelewa na tungejua jinsi tu ya kuwa wanaume na wanawake bora, wavulana kwa wasichana. Tukijua ya kwamba lile lango kuu kule mautini, ya kwamba, kila wakati moyo wetu unapopiga, tunafikia tu pigo moja karibu zaidi na lango hilo ambalo sote tutaingilia. Na halafu tukijua, ya kwamba, baada ya sisi kuingia mle ndani, hakuna hata nafasi moja tena ya kufanya upatanisho. Kamwe hatutaweza tena kuwa na fursa hii ambayo tunayo sasa hivi. Na bila kujua ni lini hasa tutakapovuka mstari huo, Ee Mungu, njoo kwetu upesi na utulete kwenye hisia tunazopaswa kuwa nazo, na tujue jinsi ya kukukaribia Wewe, na kuitetea kesi yetu mbele Zako na kuomba rehema. Tujalie, Bwana.

48 Sisi ni watu wahitaji. Sisi ni kondoo, tukimwita Mchungaji ambaye atatuongoza maishani, na kupitia katika bonde la uvuli wa mauti. Kama Daudi, wa kale, alivyosema, "Sitaogopa nitakapofika mahali hapo," kwa sababu Mchungaji ataniongoza moja kwa moja kupitia mahali hapo, mpaka miguu yetu itakapotulia juu ya Ufuko huo mtukufu, ambapo uzee na magonjwa na huzuni na mauti vitatukimbia, nasi tutakuwa huru, Huko, milele.

49 Nena, Bwana. Maskini kipenzi huyu mwenye macho maangavu wa mtu fulani, anayeketi hapa mbele yangu, katika kiti hiki cha magurudumu; kamwe siwezi kuyaondoa macho yangu kwake leo hii; amelemazwa kabisa na hii polio, yale ambayo yule mwovu amemfanyia. Ee Mungu, lete ukombozi kwa

huyo mtoto mpendwa. Tujalie, Bwana. Sio kwake tu, bali kwa wengine hapa ambao wanangojea. Jalia Roho Wako Mtakatifu awainue juu sana, asubuhi ya leo, hata watapita kila mtetemo wa shaka na kila kizuizi cha dhambi, ili Roho Wako Mtakatifu aweze kuwajilia na kuwaponya. Tujalie mambo haya, Bwana. Kwa kuwa tunaomba baraka hizi kwa ajili ya utukufu Wako, katika Jina la Mwanao, Yesu Kristo. Amina.

50 Sasa, nimechagua kwa ajili ya somo asubuhi ya leo. . . Na ninyi jamaa wadogo mnisamehe, kwa kutumia muda wote kwa watu wazima, na darasa lenu halipo hapa, halitakuwapo asubuhi ya leo. Lakini nataka msikie, pia, ninachotaka kusoma. Nami ninataka kusoma, asubuhi ya leo, kutoka katika Samweli wa Kwanza, mlango wa 3.

51 Nami ninataka kuchukua kwa ajili ya somo: *Isikie Sauti Yake*. Hilo litawafaa wasichana wadogo na wasichana wakubwa, na wavulana wadogo na wavulana wakubwa, wote. Kumbukeni hilo somo: *Isikie Sauti Yake*.

52 Sasa, ninyi mnaoyafungua Maandiko, kwenye Samweli wa Kwanza, mlango wa 3, hivi ndivyo inavyosema kwenye mistari kumi ya kwanza.

> *Basi mtoto Samweli akamtumikia* Bwana *mbele ya Eli. Na neno la Bwana lilikuwa adimu siku zile; hapakuwa na mafunuo dhahiri.*

53 Loo, jinsi ningetaka kukaa pale kwa dakika moja, labda wakati mwingine. Limenigusa tu. Hebu nikisome tu tena, kifungu hicho.

> *Basi mtoto Samweli akamtumikia Bwana mbele ya Eli. Na neno la Bwana lilikuwa adimu siku zile;* kwa kuwa *hapakuwa na mafunuo dhahiri.*

54 Mnaona ono ni nini, basi? Ni Neno la moja kwa moja la Bwana. Mnaona? Na Neno la Bwana lilikuwa adimu.

> *Ikawa wakati huo, Eli alipokuwa amelala mahali pake, tena macho yake* yameanza *kupofuka, hata asiweze kuona;*
>
> *Na kabla taa ya Mungu haijazimika bado katika hekalu la Bwana, palipokuwa na sanduku la Mungu, na Samweli alikuwa amelala;*
>
> *Bwana akamwita Samweli, naye akajibu, Mimi hapa.*
>
> *Akamwendea Eli kwa haraka, akasema, Mimi hapa; kwa maana uliniita. Akasema, Sikukuita; kalale tena. Naye akaenda,* akalala *tena.*
>
> *Na Bwa-. . . Bwana akaita mara ya pili, Samweli. Naye Samweli akaondoka, akamwendea Eli, akasema,* Mimi *hapa. . . Mimi hapa; kwa maana uliniita. Akajibu, sikukuita, mwanangu; kalale tena.*

*Basi Samweli alikuwa hamjui* B*WANA* *bado, na neno la* B*WANA* *lilikuwa bado halijafunuliwa kwake.*

B*WANA* *akamwita Samweli mara ya tatu. Naye akaondoka akamwendea Eli, akasema, Mimi hapa; kwa maana uliniita. Ndipo Eli akatambua ya kuwa* B*WANA* *ndiye aliyemwita yule mtoto.*

*Kwa hiyo Eli akamwambia Samweli, Enenda, kalale: na itakuwa, akikuita, utasema, Nena,* B*WANA*; *kwa kuwa mtumishi wako anasikia. Basi Samweli akaenda akalala mahali pake.*

B*WANA* *akaja, akasimama, akaita vile vile kama kwanza, Samweli, Samweli.* Ndipo *Samweli akasema, Nena; kwa maana mtumishi wako anasikia.*

55 Sauti ya Mungu! Kuisikia Sauti Yake katika siku hiyo lilikuwa ni jambo adimu. Mnaona, hapakuwa na maono dhahiri. Na lilikuwa ni jambo adimu, Sauti halisi ya Mungu, kwa maana watu walikuwa wameondoka. Walikuwa na kanisa, katika siku hiyo, ambalo kamwe halikuzifuata amri za Bwana. Walikuwa na m—mhudumu jina lake Eli. Naye alikuwa amemwacha Mungu, kwa kufundisha tu kanuni ambazo watu walitaka kuamini. Ikiwa hiyo haiendi sambamba na siku hizi! Aliwafundisha tu watu, naye a—alichagua iliyo bora sana, naye aliwaacha wanawe wachukue nyama iliyo bora sana kutoka huko, viopoo, kutoka kwa—kwa sadaka. Basi pakawa tu ni mahali ambapo sadaka ilikuwa ndilo jambo kuu. Naye Samweli, akazembea tu jinsi alivyozishika amri za Bwana. Nalo Neno halisi la Mungu lilikuwa ni kitu adimu.

56 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Tunaenda kanisani na tunakuta watu wakiingia na kuwa na miradi mikubwa, “Tunataka kufanya dhehebu letu, mwaka huu, kuongezeka kiasi *hiki*. Leta barua yako kutoka kwa hilo kanisa lako lingine, ukaungane nasi.” Na misemo kama, “Milioni moja zaidi katika mwaka wa ’44.” Na mengine yote kama hayo, wakilia, wakijaribu kuongezeka walishinde hilo dhehebu lingine. Na kwa kufanya hivyo, tumelegeza kamba, za Biblia. Tumeondoka, tukaanza kufundisha mambo mengine.

57 Manabii walinena juu ya siku hizi, ya kwamba wakati, “Wao, kwa mafundisho, watafundisha mafundisho ya mwanadamu wala si Mafundisho ya Mungu.”

58 Nasi tumeona mengi sana ya hayo, na imeendelea kwa muda mrefu sana, mpaka, leo hii, Neno la Bwana ni kitu adimu, hata mtu anaweza kuja na kusema, “BWANA ASEMA HIVI.” Sasa, tumekuwa na uigaji mwingi wa hilo. Shetani kweli yuko kazini. Na miaka mingi iliyopita, watu waliogopa kusema hivyo isipokuwa ilikuwa ni Bwana. Lakini, siku hizi, hawajali kabisa. Lakini ni jambo adimu kuisikia Sauti ya Bwana, na kupata mtu anayeweza kusema, “Bwana alinena nami.” Unaona hilo

miongoni mwa watu, tena, kwamba ni vigumu kwao kusikia wakati ambapo wanasema, "Bwana alinena nami."

59 Wakati, wanaume na wanawake walikuwa wakisali usiku kucha, na nyumba zao ziliwekwa katika utaratibu, kwa Kitabu cha Bwana, naye Mungu alikuwa wa kwanza nyumbani mwao.

60 Mnaona, tuna mambo mengi sana mbele ya Bwana. Huwezi kuwa na mkutano wa maombi, kwa sababu Bw. Godfrey anaendelea usiku wa leo. Huwezi kuwa na mkutano wa maombi, kwa sababu *Tunampenda Susi* kinaendelea usiku wa leo. Au, namna fulani ya upuuzi wa kipumbavu kama huo, unaochukua wakati wetu, wala hatuna wakati wa kuisikia Sauti ya Bwana. Na wale wanaodai kuwa Wakristo, wanapiga tu magoti, kwa maombi mafupi namna hii, ya kujibunia, "Bwana, nibariki mimi na familia yangu, na utushughulikie. Usiku mwema." Halafu kesho yake asubuhi, wanaamka na kusema, "Tuongoze tu siku nzima. Siku njema."

61 Tunapaswa kumngojea Bwana. Mnaona, tunashikilia kuzungumza. Hatumpi nafasi ya kutujibu. Kwamba, laiti tungeomba, na tuombe mpaka nafsi yetu ije Uweponi mwa Mungu, halafu tutulie tu na kuisikiliza Sauti Yake.

62 Lakini kuna sauti nyingi sana, siku hizi, ambazo huondolea mbali Sauti ya Bwana kutoka kwetu. Kuna sauti ya anasa. Watu wengi sana wanaisikiliza hiyo, ambapo wanaweza kwenda na kuwa na wakati mzuri. Na wengi wao wanadai kuwa Wakristo. Aina fulani ya roki inakuja, kamwe hawawezi kusikiliza yaliyo ya kiungu. Wanasema, "Vema, mimi ni Mkristo, ninapaswa kusoma kifungu kimoja katika Biblia leo. Naam, 'Yesu akalia.'" Ndivyo hivyo. Endelea. Lakini basi kwa kweli kupiga magoti na kuomba, wanayo mambo mengine mengi sana ya kufanya. Kuna sauti nyingi sana ulimwenguni, mambo mengi sana ya kuvutia usikivu wetu kutoka kwa Mungu.

63 Na jana, wakati mimi na mke wangu tulipokuwa tumekimbia kwenye supamaketi, kununua vyakula. Nami nilikuwa nikiharakisha kwa sababu nilikuwa nimechelewa kufanya miadi na kadhalika, na kuharakisha sana. Basi kulikuwako na mvulana mdogo amesimama pale, anasinzia, ndipo maskini msichana mdogo akaja pale amevaa maskini suruali, ambayo ilikuwa ya mwanamume fulani. Ilibidi iwe, kwa maana zilishonwa kwa ajili ya wanaume.

64 Nayo Biblia inasema, "Ni chukizo machoni pa Mungu, kwa mwanamke kuivaa."

65 Huku amejipaka rangi hizi nyingi sana hapa za midomoni, na macho yake yakiwa yanasinzia, akasema, "Yuko wapi *nanii*?" kwa yule mvulana mdogo.

Akasema, "Unanitarajiaje kujua?"

66 Msichana huyo akasema, “Unakumbuka, sikuingia humu mpaka saa kumi na mbili asubuhi hii.” Wala hakuwa na zaidi ya umri wa miaka kumi na miwili.

67 Sasa, Yesu, akiwa na umri wa miaka kumi na miwili, ambaye alikuwa mfano wetu, alisema, “Je, hamjui ninapaswa kuwa katika shughuli za Baba Yangu?”

68 Si ajabu Sauti ya Mungu ni kitu adimu siku hizi. Imezimwa, na sauti nyingi mbalimbali, vitu vingi sana vinavyoififiliza na kuiondosha. Imefikia mahali hata inazififiliza hisia zetu, mpaka hatuwezi kuisikia Sauti ya Mungu. Hisia zetu, za mahali tunapopaswa kujitikisa wenyewe, na kutambua kwamba nyinyi ni wanaume na wanawake, nanyi ni viumbe vya Mungu, nanyi mliwekwa hapa ili kumtumikia Yeye. Lakini sauti ya Shetani na manabii wa uongo, “Loo, kuwa wa kisasa!”

69 Kama nilivyokuwa nikizungumza siku chache zilizopita, nilikuwa nikija kanisani, ndipo nikaifungua redio yangu. Ndipo nikasikia kipindi kutoka Louisville, ambacho kilisema kwamba walikuwa wakiwafundisha watoto wao, makanisani, kunywa pombe tu kwa kiasi. Wakiwafanya wa kisasa, wasije wakanywa kupita kiasi.

70 Loo, wanapaswa kuwafundisha Kristo, sio kunywa pombe. Na hiyo itavunja na kuharibu na kuangamiza nyumba yoyote. Sauti ya Mungu ingewezaje kunena miongoni mwa familia ambayo imelewa wiski, na akili zao zimepooza kwa kuvuta sigara na ulevi, na shamrashamra za ulevi usiku kucha?

71 Watu wamngojeao Mungu, huja katika Uwepo Wake. Na kuja katika Uwepo wa Mungu ni kama tu kutoka asubuhi na mapema, wakati umande na maua yote ni matamu. Unapokuja mbele ya mtu kama huyo, unajua wamekuwa pamoja na Mungu.

72 Mke wangu aliniambia, tukija huku, asubuhi ya leo. Alisema, “Billy, simaanishi kusema haya kumsifu mtu yeyote. Lakini,” akasema, “jana usiku,” ninaamini, au mojawapo ya usiku, akasema, “Niliketi karibu na mmoja wa maskini wale wanawake wa Kiamishi, na maskini mama mmoja aliyevaa kofia kichwani mwake.” Akasema, “Nawe ungeweza kujua mwanamke huyo alikuwa pamoja na Yesu, kwa maana alikuwa mtamu. Nafsi yake ilikuwa tulivu. Macho yake yalikuwa maangavu.” Hakuna dhambi au kitu cha kujificha nyuma, wala chochote kile. Amekuwa katika Uwepo wa Mungu. Hisia zake hazikuwa zimefifilizwa, kwa wiski na tumbaku, na kila namna ya mambo ya ulimwengu. Alikuwa ameburudishwa kutoka katika Uwepo wa Mungu, akiisoma Biblia yake, akijifunza Neno la Mungu.

73 Lakini, sisi Wamarekani wa kisasa, tunachofanya! Na manabii wa uongo nyuma ya mimbara wanasema hiyo ni sawa. Mimi niko katika dhana ya kusema hivi. Kama nimekosea, Mungu anisamehe. Nimeshawishika kwamba wengi wao hawamjui Mungu. Wala kusanyiko halitawahi kuishi juu

zaidi kuliko mchungaji wake. Si ajabu Maandiko yanasema, "Wachungaji hawa, jinsi walivyolitawanya kundi! Ole wao. Wao ni matawi ambayo hayazai matunda, ambayo yatang'olewa na kuchomwa moto."

74 Mambo mengi sana ya kufifisha hisia za watu siku hizi! Loo! Lakini katikati ya hayo yote, licha ya kila sauti ya kufifisha na kila sauti iliyopo ulimwenguni siku hizi! Baadhi yao, sauti za anasa. Baadhi yao ni—ni sauti za dhambi, ili kuwashawishi watu. Lakini licha ya kila moja ya hayo, Ukweli wa Mungu ungali upo, "Yeye atakayeisikia Sauti Yangu na kunifuata!" Wanaume na wanawake watakaoisikia Sauti ya Mungu: Mungu angali anangoja kunena na kila mtu binafsi watakaofungua masikio yao kuisikia Sauti ya Mungu.

75 Ikiwa mtu, yeye ni nani, na mchungaji. . .Mara nyingi, watu wanasema, "Kwani hungeweza kufanya *hivi*? Hungeweza kukimbia *huku*? Hungeweza kufanya *hivi*?" Loo, ninapenda kufanya hivyo. Lakini sina budi kukaa katika Uwepo wa Mungu kama nitafanya jambo hilo sawasawa. Kisha watu wanasema, "Loo, Ndugu Branham ni mmoja wa hawa wanaojitenga." Sivyo hivyo. Ninawapenda watu, lakini kuna maelfu yao. Bali sina budi kukaa pamoja Naye, nipate kujua kile ambacho Yeye angenitaka niwaambie. Mahali fulani, sikilizeni tu, Yeye atakuwa na jambo fulani kwa ajili yenu, ambalo anawataka mjue.

76 Mchungaji, kamwe usiwe na shughuli nyingi kupita kiasi ila ambavyo unaweza kukaa katika huo Uwepo na kuisikia Sauti Yake. Mungu sikuzote hulitimiza Neno Lake. Na haijalishi nyakati zinaweza kuwa mbaya jinsi gani, kanisa lako linaweza kufundisha kiasi gani dhidi yake, Yesu Kristo bado yuko tayari kunena ile Sauti ndogo tulivu kwa mtu yeyote ambaye atamsikiliza. Angali yuko tayari kufanya hivyo, ikiwa tutajituliza.

77 Lakini tunakimbilia ndani, tumevurugika, na kusema, "Aisee, mchungaji, naweza kujiunga na kanisa hili?"

"Umetoka kanisa gani?"

"*Fulani-wa-fulani*."

"Vema, tuletee barua yako." Loo, jamani!

"Je, ninaweza kujiunga na kanisa hili?"

78 "Loo, ndiyo. Njoo huku, nasi tutakunyunyizia kidogo, kwa maji, na kuweka jina lako kwenye kitabu. Nawe utapewa mkono wa kuume wa ushirika."

79 Vema, Chama cha Masoni kina utaratibu bora kuliko huo. Ni kweli. Chama cha Masoni na vyama vingine vyote ni sawa, lakini bado si nyumba ya Mungu. Humo ndimo Mungu anamozungumzia. Vyama hivyo vinajaribu kukupa maadili, lakini Mungu hukufanya kuwa mwadilifu kwa Yesu Kristo,

Mwanawe. Sasa, kuna kanuni ya maadili kwake; Mungu ana Kuzaliwa upya kwa ajili yako.

80 Lakini isikieni Sauti Yake ndogo tulivu. Kila mmoja wenu ninyi watu mnaokiri kuwa Wakristo, tulieni mbele Zake. Msiruhusu kufua nguo kuzuie. Msiruhusu kazi izuie. Msiruhusu chochote kizuie. Usiruhusu mtu yeyote kujua unachofanya. Nenda tu mbele Zake. Ingia msituni mahali fulani. Nenda kando ya barabara. Ingia kwenye chumba cha siri na ufunge mlango. Watoto wanapoenda shuleni, hapo piga magoti. Umesikia kila aina ya sauti kila mahali, lakini piga magoti tu na ukae hapo mpaka hizo sauti zimenyamazishwa na umeanza kuinuliwa juu. Itakubadilisha. Itakufanya kuwa tofauti, kama ilivyomfanyia huyu mtoto Samweli. Itakufanyia kitu ikiwa utafanya tu. Sasa, itakufanya kile unachopaswa kuwa. Itakufanya aina ya Mkristo unayepaswa kuwa.

81 Sasa hebu turudi nyuma kutoka katika siku hizi za kisasa, mpaka siku ambazo zimepita. Hebu turejee kwenye siku za nyakati za mwanzoni. Nayo Sauti hii ya Mungu imewajia wanadamu katika nyanja zote za maisha, katika nyakati zote. Haijalishi kama wewe ni mkulima, kama wewe ni fundi viatu, chochote ulicho, Mungu angali ananena. Kama wewe ni mwenye dhambi, kama wewe ni kahaba, malaya, kama wewe ni mlevi, kama wewe ni (nini?) mshiriki wa kanisa la mtaa, wa kawaida—kawaida, chochote uwezacho kuwa, Sauti ya Mungu ingali inangojea kunena nawe.

82 Ninawazia sasa juu ya Musa, alipokuwa tayari ana umri wa miaka themanini, naye alikuwa na miaka themanini ya mafunzo ya kitheolojia. Naye aliyajua Maandiko; aliyafahamu vyema. Naye alikuwa ameahidiwa, ya kwamba atakuwa mkombozi wa watu wake. Lakini, hata hivyo, kuyajua tu Maandiko na kuwa m—mshiriki wa kawaida wa kanisa hilo la kisasa katika siku hiyo, alichukua jambo hilo mikononi mwake mwenyewe na kujaribu kulifanya. Alimwua Mmisri. Unaona unachofanya bila kumsikiliza Mungu? Unavuruga tu mambo.

83 Na wakati ibilisi, asubuhi ya leo, angesema, “Usibatizwe.” Mwingine angesema, “Loo, fanya hivyo baadaye.” Mwingine angesema, “Afadhali uhakikishe unajua unachofanya.” Na huyo mwingine aseme, “Utajikosesha starehe.” Njia pekee ya kutatua hilo, ni kuliendea Neno la Mungu nalo. Lakini watu, siku hizi, hawaonekani kutaka kufanya hivyo.

84 Basi, Musa, alikuwa ameenda kwa walimu bora zaidi, lakini walikuwa wamekuwa wa kawaida na baridi. Alikuwa amesikia hadithi aliyoambiwa na mama yake, jinsi alivyofichwa kwenye manyasi, na jinsi ambavyo mamba wakubwa wasingeweza kumshika. Jinsi ambavyo, mtoto huyo mchanga alivyokuwa akielea mtoni. Ambamo . . .

85 Maskini mamba hao walikuwa wanono tu. (Hii ni kwa ajili ya watoto wadogo.) Walikuwa wanono, kutokana na kuwala hao watoto wachanga. Walikuwa na vizee wanawake wenye pua zilizopinda, polisi wanawake, kamwe hawakuzaa mtoto, hawakujua jinsi upendo wa mtoto mchanga ulivyokuwa. Mbona, wao wanaenda tu huko nje na kuwachukua na kuwaua hao watoto wachanga, na kuwatupa mtoni. Maskini mamba hao walikuwa wamenona kabisa, kwa kuwala hao watoto wachanga.

86 Na, hata hivyo, Mungu aliweka juu ya moyo wa huyo mama kumweka mtoto wake mchanga mumo humo mautini. Hivi hamwoni ilikuwa ni mfano wa Kristo? Aliingia moja kwa moja mautini. Na kila mmoja wa hao mamba wakubwa angekuja kwenye kikapu hicho kidogo kinachoshuka mtoni. Mnajua kwa nini hawakuweza kufanya hivyo, kwa nini wasingeweza kumla mtoto huyo mchanga? Kulikuwako na Malaika aliyekuwa ameketi pale. "Ondoka hapa."

87 Kwa nini? Mungu huwaagiza Malaika Zake kuwachunga watu Wake. Usiogope, mpenzi. Mungu anakulinda. Huenda ibilisi akajaribu kukufanyia jambo fulani, lakini Mungu ni mkuu zaidi. Unaona?

Kwa hiyo, inawalazimu mamba kukitoroka maskini kikapu hicho.

88 Na, hata hivyo, Musa alijua mambo haya yote. Na, hata hivyo, baada ya miaka arobaini ya mafunzo, na kisha jangwani, bado alijaribu kuchukua kitu hicho, mikononi mwake.

89 Tunajua Biblia, yale ambayo Mungu anasema tufanye, na hata hivyo tunasema, "Vema, sasa, tutafanya Hili liwe *hivi*. Ni, ninii tu, siku za miujiza hazipo tena. Tunajua hatuamini kwamba tunaziona tena, na tunaamini siku za miujiza zimepita. Na kunyunyiziwa ni kuzuri tu kama kuzamishwa. Na 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu' ni zuri tu kama Jina la Bwana Yesu. Na kwa hivyo tutaninii tu . . . Wengine wao wanakwenda hivyo, kwa hiyo tutafanya tu hivyo, pia."

90 Musa alikuwa mwanajeshi. Naye alifikiri kwamba jinsi alivyofunzwa, kama mwanajeshi, kwamba angeweza tu kuwaua hao Wamisri kwa mkono wake. "Ni sawa tu na kufanya yale Mungu aliyofanya." Je, uliwahi kufikiria jambo hilo? Kila mtu anamhukumu Musa kwa kumwua mtu mmoja. Naye akarudi kule chini akiwa na upako wa Roho Mtakatifu na kukiua kitu hicho chote, hakuna mtu aliyesema lolote kuhusu hilo. Aliliua jeshi lote la Farao, lakini Mungu alikuwa ndani yake. Mungu hakuwa katika yale ya kwanza.

91 Na ndipo Musa, akiwa ameshindiliwa tu theolojia ya kanisa, alikuwa awe halifa wa farao. Nasi tunamwona, bado hamjui Mungu.

92 Lakini asubuhi moja, upande wa nyuma ya jangwa, mzee mwenye umri wa miaka themanini, masharafa yake

yakining'inia chini kabisa, aliona kichaka kinachowaka moto. Naye akageuka aone kilichokuwa kikiendelea. Basi alipokaribia kile kichaka, alisikia Sauti. Ilimbidi Mungu kumnyamazisha kwa muda wa miaka arobaini, kabla hajaweza kuzungumza naye. Nasi hatutatulia dakika kumi, Mungu aweze kunena nasi, pamoja na ngurumo na uvumi wote tulio nao wa siku hizi.

93 Na hata hivyo, Musa, baada ya miaka arobaini, alisimama pale, na Mbele ya kile kichaka. Na Sauti hiyo moja iliyomwita, alijua zaidi juu ya Mungu katika dakika tano, baada ya hapo, kuliko aliyofundishwa na miaka yote themanini ya mafunzo. Ilimfanya mtu tofauti.

94 Itakufanya mwanamume na mwanamke tofauti, kama tu ukisimama kimya muda mrefu vya kutosha kusikia Sauti Yake, kama Samweli alivyofanya. Simama kimya. Usisisimkwe. Ukitaka kitu kwa Mungu, mwombe; kisha usimame kimya na kusikiliza, uone atasema nini juu yake. Fungua tu moyo wako, useme, “Vipi kuhusu hilo, Bwana Yesu?” Baki tu hapo. Asipojibu saa tano za kwanza, basi subiri zingine. Asipojibu leo, basi atajibu kesho. Asipojibu wiki hii, atajibu wiki ijayo. Kaa hapo mpaka atakapojibu.

95 Sikia Sauti Yake ikijibu, moyoni mwako, na kusema, “Naam, Mimi ndimi Bwana nikuponyaye.” Ndipo yote yamekwisha. Unaweza kutulia basi. Unaona? “Mimi ndimi Bwana nikusameheye dhambi zako zote. Sasa nenda zako na usitende dhambi tena. Sikuhukumu.” Ndipo unaweza kuwa huru. Uko sawa. Lakini unataka kuwa na uhakika ya kwamba uliisikia Sauti hiyo ikinena. Musa aliisikia. Alikuwa mtu aliyebadilika.

96 Mwangalie Isaya, nabii. Akiwa kijana, aliisha fanikiwa. Yule Mfalme mkuu Uzia aliyependelewa, katika siku hizo, mtu mwenye haki, mtu mwema. Alimpenda Isaya, kwa maana alijua alikuwa nabii. Na kwa hivyo aliegemea tu kwenye mkono wa mfalme. Kila kitu alichotaka, mbona, Uzia alimpa. Na kila wakati alipotaka chochote, mbona, huyo mfalme mwema angempa. Lakini ilifika wakati ambapo huyo mfalme alikufa.

97 Ufanisi sikuzote huwaangamiza watu. Hilo ni jambo gumu kusema. Lakini ufanisi humpeleka mtu mbali na Mungu. Mungu alinena mahali pamoja, katika Biblia, jambo kama hili, Naye akasema, “Nilipokubariki, na kukupa mengi. Ulipokuwa maskini wala hukuwa na kitu, nilikuja kwako, nawe ukanisikia na kunitumikia. Lakini nilipokubariki na kukupa mengi, ndipo ukanipa kisogo.” Hivyo ndivyo Marekani imefanya, wamegeuza vichwa vyao.

98 Hivyo ndivyo makanisa yalivyofanya. Unaweza kuketi pembeni, na kuwa na majengo makubwa mazuri, na mamilioni ya dola kwa. . .yanawekwa ndani yake, na kila kitu rahisi tu kinavyoweza kuwa. Si ajabu huna muda wa kuisikia

Sauti ya Mungu. Lakini ngoja mpaka saa ifike ambapo hayo yataondolewa, ndipo utatamani kuisikia. Kila kitu kiko shwari sasa, lakini saa inakuja ambapo haitakuwa hivyo.

99 Kwa hiyo, Isaya, angeweza kuegemea mkono wa mfalme. Naye alikuwa ni kijana mwanamume aliyependelewa, na roho nzuri ndani ya kijana huyu, kwa hiyo mfalme alimpenda. Basi siku moja, hayo mategemeo yaling'olewa chini yake. Yule mfalme akafa. Na wakati mfalme alipokufa, basi ilimbidi Isaya ajitegemee. Ndipo akaanza kutazama huku na huku, ndipo akagundua ya kwamba kila mtu hakuwa kama yule mfalme.

100 Utafukuzwa, moja ya siku hizi, kutoka kwenye haya makundi yasiyo ya kimadhehebu kama hili. Utakuja wakati ambapo itakubidi kuwa mfuasi wa dhehebu fulani, la sivyo hutaweza kuabudu. Kama mjuavyo, Maandiko yanasema itakuwa hivyo. Kwa sasa wanakudhihaki tu. Lakini kuna wakati ambapo kutakuwa na kususiwa, kwa maana alama ya mnyama lazima ije. Ama utakuwa mwanachama wa mwungano wa makanisa, yule mnyama kama vile alivyo huko Rumi, la sivyo hutaabudu hata kidogo. Hivyo ndivyo Maandiko yanavyosema. Hapo ndipo itakubidi kulia kama Isaya alivyofanya.

101 Naye akashuka hekaluni, ndipo akatambua basi. Akainua mikono yake na kusema, "Ee Bwana, mimi ni mtu mwenye midomo michafu." Unafikiri wewe ni mwema, lakini ngoja mpaka wakati huo utakapokuja. "Ninaishi miongoni mwa watu wenye midomo michafu." Alifanya nini? Alipata shauku kuu.

102 Basi unapokuwa na shauku kuu kuhusu jambo hili, kitu fulani kitatukia. Hujapata shauku kubwa vya kutosha. "Loo, vema, nilijiunga na kanisa. Hilo latosha." Lakini huna budi kulionea shauku kuu. Unapaswa kumhitaji Mungu kweli.

103 Yesu alisema, "Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana watashibishwa."

104 Lakini mradi umeridhika na mambo ya ulimwengu, Mungu anawezaje kuzungumza nawe? Unasema, "Mungu hajawahi kusema nami." Kwa nini? Anataka kufanya hivyo. Lakini umeshindiliwa mambo ya ulimwengu kupita kiasi. Hiyo ndiyo shida yetu siku hizi. Tunaweka muda wetu wote kwenye mambo ya ulimwengu, na anasa za ulimwengu, wala hatumpi Mungu wakati wowote. Ni kweli.

105 Sasa, tunaona ya kwamba Isaya aliona shauku kuu. Naye akapaza sauti, na kuungama dhambi zake, na kuungama dhambi za watu. Alipomaliza kukiri, alisikia kelele juu yake. Ndipo alipotazama juu, kulikuwako na Makerubi, wakiruka huku na huku kote jengoni. Mabawa juu ya nyuso Zao, na mabawa juu ya miguu Yao, na kuruka kwa mabawa, wakilia, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi."

106 Jambo fulani lilikuwa likitendeka. Isaya akapatwa na shauku kuu. Mungu akaingia kazini. Ndipo Isaya akalia kwa

sauti kuu, "Nina midomo michafu," kwa maana Sauti ilikuwa imenena hivi punde. Ikambadilisha.

107 "Ni nani atakayekwenda kwa ajili Yetu?" ikasema Sauti. "Nani ataenda? Ni nani aliye tayari kusimama katika pengo, miongoni mwa kundi hili la wanatheolojia? Ni nani atakayekwenda katika siku hii, na kutangaza kwamba Mimi ningali Mungu? Ni nani atakayekwenda na kuhukumu uchafu wao? Ni nani atakayebomoa madhehebu yao na kujenga tena nguvu za Mungu aliye hai? Nani ataenda?"

108 Isaya akasema, "Bwana, kabla sijaenda, sina budi kubadilishwa." Baadhi ya hofu hizi ndogo ndogo na mivurugiko ilibidi zimwache.

109 Ndivyo itakavyokuwa kwa kila mtu anayeitwa na Mungu! Huna budi kuzaliwa mara ya pili, kubadilishwa na kufanywa upya. Sio mawazo; lakini kutoka moyoni mwako, kitu ambacho kweli hufanyika. Ndipo mmoja wa Malaika . . . "Ukiomba, utapokea."

110 Mmoja wa Malaika akaenda kwenye madhabahu ya shaba, naye akatwaa yale makoleo na kunyosha mkono akatwaa kaa la Moto ulio hai, akamkimbilia Isaya na kuliweka kinywani mwake. Akasema, "Sasa wewe ni safi. Nenda, nena Neno." Isaya alibadilika baada ya kuisikia Sauti hiyo.

111 Kisha katika miaka yake ya mwishoni, akaandika Biblia nzima. Alianzia kwenye Mwanzo na kuishia katika Ufunuo. Kuna Vitabu sitini na sita vya Biblia; kuna milango sitini na sita ya Isaya. Kwa nini? Kwa sababu alipata shauku kuu, katika wakati ambapo aliona ilihitajika zaidi.

112 Danieli, kule chini Babeli, kama tulivyonena habari zake jana usiku. Alikuwa amekusudia moyoni mwake kwamba hatajitia najisi kwa mafundisho ya Babeli. Lakini siku moja, kule chini, Danieli akawa na haja. Naye alijua alitaka kuisikia Sauti ya Mungu, hata hivyo alikuwa na Maandiko. Lakini alihitaji kuisikia Sauti ya Mungu. Ndipo akashuka kwenye mto *fulani*. Naye hakushuka tu kule chini na kuegesha gari lake la farasi na kupiga magoti kwenye manyasi, na kusema, "Bwana Mungu, nataka kukusikia Wewe. Uko wapi?" Hapana. Hulifanyi hivyo. Isaya alikuwa amechukua gari lake la farasi, na waendeshaji, na alikuwa ameshuka hadi mtoni na kuwarudisha nyuma. Alikuwa anaenda kukaa mpaka asikie. Hiyo ndiyo njia. Alilionea shauku kuu.

113 Ilimbidi aondoke moja kwa moja kutoka kwenye askari wote, na wanajimu wote, na mamajusi, madaktari wote wa theolojia, na kadhalika, waliokuwa wakijaribu kumwambia, "Hivi! Fanya *hivi*, Danieli. Fanya *hivi*, Danieli." Lakini akawaondokea hao wote. Hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya. Ndipo akashuka mtoni, na akakaa huko kwa muda wa siku ishirini na moja, akishindana mweleka na Malaika wa Bwana.

114 Lakini tunaambiwa kwamba alitazama nje juu ya maji. Hapo akamwona Malaika amesimama, huku amekanyaga nchi na bahari kwa mguu Wake. Akainua mikono Yake na kuapa kwa Yeye aliye hai milele na milele, "Wakati mambo ambayo Danieli aliona yatakapotimia, wakati hautakuwako tena." Alikuwa amecheleweshwa siku ishirini na moja kwa sababu ya uovu wa nchi.

115 Na kama alicheleweshwa siku ishirini na moja kwa sababu ya uovu wa nchi hiyo katika siku za Uajemi, Yeye angekuwaje katika siku hii? Angecheleweshwa kwa muda gani? Lakini imani hiyo isiyokufa, hiyo njaa na shauku moyoni mwa mwanadamu, ambayo haitamwambia Mungu hapana, bali itashikilia mpaka Mungu atakaponena kutoka Mbinguni. Huwezi kucheza na hii, na Injili hii. Sio ya kuchezewa. Ni lazima ilenge shabaha, mara kumi kwa kumi. Haina budi kuwa kamilifu, la sivyo si sahihi na haitafanya kazi. Haina budi kuwa kamilifu. Danieli aliomba.

116 Tunaona katika Biblia, yapata mlango wa 8, mlango wa 7 au wa 8 wa Kitabu cha Matendo, kwamba, maskini Farisayo mmoja, wa mtindo wake mwenyewe jina lake Sauli. Loo, alikuwa mwanatheolojia, vema. Alikuwa ameketi chini ya mafundisho ya Gamalieli naye alikuwa na Maandiko yote, moja kwa moja jinsi yanavyopaswa kuwa, kulingana na wanatheolojia wa siku hizo, loo, wa mtindo wao wenyewe na wenye kujiendeleza wenyewe. Naye akawaona watu wakifanya jambo ambalo lilikuwa la kiroho, wala theolojia yake ya kujibunia isingeweza kuambatana na Hilo.

117 Ni mfano ulioje wa siku hizi! Mwaminifu na mkweli moyoni mwake, kama vile watu wengi walivyo, wanafikiri kwamba watu waliozaliwa mara ya pili wana kichaa. Wanafikiri ya kwamba uponyaji wa Kiungu na nguvu za Roho Mtakatifu ni jambo *wanalozungumzia*, lakini ni kweli.

118 Basi alipokuwa akienda zake Dameski, siku moja, pamoja na baadhi ya maagizo mfukoni mwake, kutoka—kutoka kwa askofu wa kanisa, kushuka kwenda kuwaangamiza kundi hilo lote la watakatifu wanaojibingirisha waliokuwa wakipiga kelele na kupiga mayowe, na—na kuruka-ruka, na kunena kwa lugha za kigeni, na—na kuponya wagonjwa. "Na, mbona, ni kundi la ibilisi," walisema wanatheolojia. "Shuka uende ukawakamate, na kuwarudisha huku katika minyororo!"

119 "Hakika. Katika utumishi wako, askofu!" Loo, jamani! Loo, alikuwa mtu mashuhuri. Alikuwa na D.D., Ph. D., mwajua. Kwa hiyo alikuwa ameruka juu ya farasi wake, naye huyo akaenda zake, ameambatana na kundi.

120 Lakini akiwa njiani, yapata saa sita adhuhuri, Kitu fulani kikambwaga chini. Naye akagaagaa mavumbini, kama mwendawazimu, akitokwa na povu. Ndipo akasikia Sauti ikisema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?" Ilikuwa ni nini?

Sio mwanatheolo-. . . theo-. . . mwanatheolojia akinena naye. Lakini Sauti kutoka Mbinguni, “Mbona unaniudhi?”

121 Naye akageuka mavumbini, na vipaji vyake vimejaa mavumbi, na machozi yakitiririka mashavuni mwake, labda. Akasema, “Bwana, u Nani Wewe?” Ndipo alipoangazia macho yake, akawa kipofu kama popo.

122 Hiyo hapo ile Nguzo kuu ya Moto imesimama mbele zake. Na Sauti ikitoka Kwake, ikasema, “Mimi ni Yesu, unayeniudhi. Mafundisho yako ya kujibunia yamekuwa mabaya.” Ilikuwa ni nini? Kulikuwako na ono dhahiri. Neno la Mungu lilifanywa halisi.

123 Loo, ndugu, hayo ndiyo tunayohitaji siku hizi, ni mengine kama hayo.

124 Nataka tu kumshukuru Bwana. Wasichana hawa wadogo, waliokuwa kwenye viti vya magurudumu jana usiku, wakija, wanakuja huku leo wakitembea, na bila viti vya magurudumu, kwa hivyo wanaenda. Uh-huh. Bwana awabariki, enyi wasichana, mnaoketi hapo. Ni nini kilichosababisha hilo? Yesu yeye yule aliyenena kwa Sauti ya kimbinguni kule nyuma, angali anazungumza hata leo.

125 “Sauli, Sauli, kwa nini unaniudhi?” Sauli alikuwa mtu aliyebadilika.

126 Na watu wanapaswa kubadilika siku hizi wakati wanapoweza kuona na kusikia Sauti ya Mungu aliye hai ikinena kama alivyofanya alipotembea Galilaya. Loo, hakika!

127 “Sauli, Sauli, mbona waniudhi?” Ni kitu gani kilichofanya hivyo? Je, alimpeleka kwenye seminari na kumfundisha theolojia mpya? Hapana, hakufanya hivyo. Alifanya nini? Alinena naye, na kulikuwako na Sauti halisi ikinena kupitia Wingu. Ilikuwa ni nini? Mungu yule yule aliyenguruma kutoka kwenye Mlima Sinai.

128 Katika mikutano, katika mahali ambapo Roho Mtakatifu huja, ninyi husikia sauti ya mwanadamu ikibadilika. Na bila kujua hata kidogo, ABC, bali Kristo anaweza kuichukua sauti hiyo na kunena siri za Mwenyezi Mungu. Inapaswa kumbadilisha kila mwanamume na mwanamke anayeketi katika Uwepo wa ninii Yake. . .?. . . “Nilisikia Sauti,” alisema. Loo, tunalala sana. Natumai sivyo, haitabidi kuwekwa dhahiri zaidi ya hapo. Lakini tunalala sana katika makanisa yetu, katika theolojia yetu, katika mawazo yetu, na katika njia zetu za maisha, mpaka tunakosa kuisikia Sauti hiyo inaponena.

129 “Loo,” wanasema, “inaweza ikawa ni telepathia. Huenda, unajua, huenda ikawa *hivi, vile*, ama *vinginevyo*.”

130 Vipi kama Musa angelisema, “Aisee, sijui kama huyo alikuwa ni pepo kwenye kichaka kile?” Huh! Hakuna swali kwa Musa, aliisikia hiyo Sauti.

131 Ukisema, "Loo, huenda ikawa ni dhamiri yangu tu inayoniambia hivyo."

132 Kama wewe ni mtoto wa Mungu, utajua ni Sauti Yake. "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu. Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu." Watajua.

133 Kulikuwako na mwingine, jina lake Petro, ambaye alikuwa ameokoka, na pia alikuwa amejazwa na Roho. Naye bado alitaka kushikilia mapokeo ya wazee. Yote ambayo angejua, yangekuwa hapa katika Neno. Ndipo siku moja, juu ya paa la nyumba, alipotaka kuyashika mapokeo ya, "Usile nyama . . . usile nyama yoyote, na sabato, na kadhalika." Kuna watu wengi wazuri wangali wanajaribu kushikilia vitu kama hivyo.

134 Ndipo siku moja alipokuwa juu ya paa la nyumba, alisikia Sauti iliyosema, "Usiite kile nilichosafisha, 'najisi.'"

135 Mungu, laiti angechukua kundi la wahubiri katika bonde hili hapa, na kuwafanya wajue ya kwamba sisi hatuna kichaa, sisi si watakatifu wanaojibingirisha, lundo la takataka. Ni Roho wa Mungu aliye hai. Nao wanaume na wanawake wamelewa kwa wema Wake. Sio uchawi wala telepathia ya kiakili. Ni Roho wa Mungu aliye hai. Yaacheni mapokeo yenu, enyi wazee, mkaisikilize Sauti ya Mungu aliye hai. Itawabadilisha. Hamtakuwa mmoja wa watesi. Mtataka kuwa mmoja wao. Kama unaweza kupita vizuizi vya mafundisho yenu yote, mpaka uweze kuelea kwenye Uwepo Wake huko ng'ambo, jambo fulani litatukia. Hutaamini siku za miujiza zimepita. Utaamini kwamba ziko papa hapa, kwa sababu mmoja utafanywa juu yako, hakika, kumbadilisha mtu. Hivyo ndivyo Sauti ya Mungu sikuzote hufanya. Inawabadilisha wanaume na wanawake na kuwafanya kile wanachopaswa kuwa; si kile ambacho shule na waalimu wamefanya, bali kile ambacho Mungu amewawekea kielelezo.

Ile Sauti, ikinena! "Nilisikia Sauti."

136 Loo, jinsi ningependa kuingia katika ujuzi wa kibinafsi. Na jinsi ambavyo mngependa kuziendea shuhuda za kibinafsi, wengi wenu ninyi wanaume na wanawake ambao mmeisikia Sauti Yake.

137 Nami ninaweza kukumbuka kuisikia nilipokuwa tu mvulana mdogo, huko chini kabisa kwenye milima ya Kentucky. Nami nilifikiri ilikuwa ni ndege ameketi juu ya mti, lakini ndege huyo akaruka akaenda. Akasema, "Usiogope, maana utaondoka hapa siku moja, na kuhamia karibu na mji unaoitwa New Albany." Niliisikia Sauti Yake aliposema, "Usivute sigara, au kunywa pombe, wala kuutia najisi mwili wako na wanawake na kadhalika. Kuna kazi ya kufanya utakapokuwa mtu mzima."

138 Loo, Yeye angali ni Bwana Mungu yeye yule. Nanyi mnamsikia, saa baada ya saa, akinena nawe katika chumba chako kidogo cha faragha, katika chumba chako cha maombi.

Anajitokeza mbele ya kusanyiko, kisha ananena na watu waziwazi. Sauti ya Mungu, ilikuwa adimu katika siku za Samweli. Ni adimu zaidi siku hizi. Kwa maana, hapakuwa na mafunuo dhahiri.

139 Petro aliisikia hiyo Sauti, Nayo ikabadilisha theolojia yake yote. Akawaendea Mataifa moja kwa moja, ambao alidhania kuwa ni kundi la watu wasio na elimu na waliofukuzwa. Lakini, Sauti ya Mungu, si mafundisho yake, Sauti ya Mungu aliye hai ilimbadilisha.

140 Na sasa moja tu zaidi. Kulikuwako na mtu mwema, wakati mmoja, katika Biblia. Jamaa aliyemfahamu Yesu, ambaye alimpenda, na kumwamini, na kumwabudu, na kucheza Naye, kisha akapanda milima pamoja Naye, na kushuka mtoni, akivua samaki pamoja Naye. Alikuwa mtu mwema. Siku moja, Yesu alipokuwa ameondoka, mauti yakaja yakavizia chumbani mwake.

141 Naye alikuwa ameliacha kanisa la kale la kiothodoksi, yeye na dada zake wapendwa, Martha na Mariamu. Nao walikuwa wametoka kwa sababu walimpenda, na kumwamini kuwa ndiye Masihi. Na kwa kufanya hivyo, kanisa lilikuwa limewatenga upesi.

142 Ndipo kijana mwanamume huyu akaugua sana mpaka akafa, naye alikuwa amezikwa, siku nne. Mafundisho ya kitheolojia yangefaa nini basi? Kanisa lake lingefaidi nini basi? Lakini kulikuwako na Sauti ya Mungu, duniani, Naye akanena na Lazaro. Naye Lazaro, mtu aliyekuwa amekufa na kuozea kaburini, aliisikia Sauti Yake, naye akatoka na kuishi tena.

143 Nilikuwa nimekufa wakati mmoja katika dhambi na makosa. Wewe ulikuwa umekufa katika dhambi na makosa. Lakini Sauti ya Mungu ndiyo iliyosema, "Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na mliolemewa na mizigo mizito, nitawapumzisha."

144 Nimeiona hiyo Sauti ikinena na kiwete, ikimnyoosha. Nimeiona Sauti ya Mungu ikinena na kipofu, nayo macho yake yakafunguka. Kwa wanaokufa, waliolemewa na kansa, kwa wenye ukoma, nikawaona wakirudi katika mwili, wakiwa na afya kamilifu tena. Nimemwona akinena na walevi sugu, na wendawazimu, na waliofukuzwa, na kundi la wasokwao, nao wakawa mabibi na mabwana, na watakatifu wa Mungu aliye hai, kwa sababu Sauti ya Mungu ilinena. Hiyo ndiyo tunayosikiliza, siku hizi.

145 Hebu nimalizie kwa kusema hivi. Utakuja wakati, ambapo nafsi yako inayozungukazunguka itakuwa imeondolewa mwilini mwako, nayo iko kwenye kikomo chake mahali fulani, ikizungukazunguka huko gizani, ama pengine kwenye vifua vya Mungu. Sauti hiyo itanena tena. Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, "Wote walio kaburini wataisikia Sauti Yake,

nao watatoka. Wengine watakuja kwenye aibu ya milele na kudharauliwa. Na wengine watatoka waje kwenye amani na furaha ya milele."

146 Asubuhi hii inaweza kuwa ndio wakati wa kufanya uamuzi wako, kama utasikiliza yale televisheni isemayo, ama yale gazeti lisemayo, ama wanatheolojia wasemayo, ama yale Mungu asemayo. Acha niwaambie, kama watu. Usisikilize kile chochote kisemacho, bali kile Mungu asemacho. Ingojee hiyo Sauti ndogo, tulivu, Naye atakubadilisha.

147 Unasema, "Ningependa kuamini, Ndugu Branham. Laiti ningeweza kuamini. Laiti ningefanya mambo fulani." Lakini huwezi. Kwa nini? Hutulii muda mrefu wa kutosha. Hufikii mahali ambapo ma—mashaka yote yamekwisha.

148 Unapoingia mahali ambapo mashaka yamepita, basi utakuwa huru, nawe unaweza kusikia Sauti ya Mungu ikinena. "Mtoto Wangu, Mimi ndimi Mwokozi wako. Mtoto Wangu, Mimi ndimi mponyaji wako. Si lazima ufanye mambo haya. Nilikufa upate kuwa huru. Lakini mradi uko hapa chini katika mtetemo huu, uliochanganyikana na sauti za kila namna, jiondoe upesi kutoka kwa hizo zote."

149 Inanikumbusha wakati mmoja ambapo nilikuwa juu milimani wakati mmoja. Wala kamwe sitasahau matukio hayo. Na hapa yapata miaka kumi iliyopita, ama si muda mrefu hivyo, nilikuwa nikimsaidia Bw. Jefferies kuwakusanya, na walipokuwa wakibeba chumvi juu ya farasi. Nami nilikuwa nikiwapeleka kwenye malambo fulani ambapo ningeweza kuiweka huko nje, ambako ng'ombe wangejua kuja. Huko nyuma kabisa, maili sabini, karibu hivyo, kutoka kwenye ustaarabu. Ama, ninamaanisha, kama maili thelathini, thelathini na tano, labda arobaini, kwenda Kremmling, Colorado, ambako unaufikia mji mdogo wenye wakazi wapatao mia saba au mia nane. Nami nilikuwa na farasi wangu, nami nilikuwa nimetoa mikoba ya matandiko, imepakuliwa. Nasi tunawaangalia. . .tunawawinda ng'ombe kwa darubini. Nami nilikuwa nimemfunga farasi wangu kwenye tawi, na trela zilikuwa nyuma yake, ambazo ni, farasi. . .farasi wa kengele yuko mbele. Nami nikapanda juu ya vilima. Na vilikuwa vizuri sana. Ilikuwa majira ya kuchipua. Nami nilikuwa nikitazama ng'ambo ya mabonde, nikitazama mawimbi madogo ya maji, kwa mbali sana. Basi nilipokuwa nikitazama, ilikuwa katikati ya alasiri, ndipo nikaona kitu ambacho kilinisisimua.

150 Nikamwona mama mzee akiwachukua watoto wake kutoka kwenye kiota chake, maskini ndege tai. Naye akapigapiga kote juu yao mpaka akawaweka kwenye mbawa zake. Nao walikuwa nje ya kiota hapo kabla. Lakini akawashusha bondeni. Hawakuwa wamewahi kuwa huko chini hapo kabla. Wanajifunza tu kuruka. Kwa hiyo, akawaachilia. Nao wakaondoka, wakila nyasi, na kuangukiana, wachangamfu

tu walivyoweza kuwa. Basi wakati nimeketi pale, nikawazia, "Sasa, hilo si ni kama tu kundi la Wakristo wa kweli, waaminio! Ni wachangamfu." Kwa nini walikuwa wachangamfu? Haikuwapasa kuogopa chochote, kwa maana mama alikuwa amerudi moja kwa moja na kuketi kwenye mwamba, kuwalinda. Lo! Hiyo inalibadilisha tu namna hiyo.

151 Unapoanza kufikiria, "Je, Mchungaji *Nanii* atafikiri nini nikimpokea Roho Mtakatifu? Askofu *Nanii* atasema nini?" Sijali watasema nini.

152 Yesu alikufa, Naye amepanda ngome za Utukufuni, na ameketi katika mbingu za mbingu. Hakuna kitu kitakachokusumbua. Jicho Lake liko juu ya shomoro, nami najua ananilinda, Naye anakulinda.

153 Ndipo akitokea, kama mbwa mwitu akija, ama kitu cha kumsumbua mmoja wa hawa wadogo, mbona, yeye... Afadhali wasithubutu. Angeweza kumshika mbwa mwitu mkononi mwake, kwa nyayo zake, ambebe juu yapata futi elfu kadhaa kisha amwachilie tu. Angesambaratika angani. Hakuna kitakachowasumbua hao vifaranga. Atahakikisha hilo.

154 Hakuna kitakachokusumbua. Usiogope kuliamini Neno Lake Mungu. Tulia tu, na uwe na imani, na kuamini. Anakulinda. Atasambaratisha chochote kinachojaribu kukusumbua. Loo, kinaweza kukushambulia, lakini hakiwezi kukudhuru. "Kwa kuwa mambo yote," Yeye analiruhusu. Isingekuwa kitu kingine chochote, "Kwa maana inafanya kazi kwa manufaa, kwa wale wampendao Bwana." Hakuna madhara yanayoweza kukujia.

155 Na kwa hiyo, baada ya kitambo kidogo, kukatokea dhoruba. Ndipo dhoruba ilipoanza, huja upesi, hao wa kaskazini, kimulimuli kidogo cha umeme na upepo huo ukija, maili sitini ama sabini kwa saa. Ndipo maskini yule tai akapiga mayowe makubwa sana, naye huyo akashuka bondeni. Na mayowe hayo, yalifanya nini? Hao tai wadogo waliijua sauti ya mama yao.

"Kondoo Wangu waijua Sauti Yangu," alisema.

156 Hatari ilikuwa karibu. Sasa, hawakujaribu kuingia chini ya vipande vinene. Hawakujaribu kukimbia waingie kwenye aina fulani ya lundo la takataka. Walimsubiri mama tu.

157 Hivyo ndivyo Mkristo anavyopaswa kufanya; kuona yale Mungu atakayofanya juu yake.

158 Basi wakati ma—maskini yule mama aliposhuka chini, hiyo miguu mikubwa namna *hiyo*, alienda tu chini kama ndege kubwa mno ikitua. Ndipo akatupa kichwa chake hewani na kupiga kelele, na kutupa mabawa hayo makubwa nje, kama futi kumi na nne, kutoka ncha hadi ncha, upana wa kutoka kwenye nguzo *hii* hadi *ile*. Hao tai watoto wote wa tai walitimua mbio tu kwa nguvu walivyoweza, wakazirukia mbawa za mama yao

moja kwa moja. Wakainama chini na kushika kwa makucha yao madogo, wakachukua midomo yao midogo, na kuuma moja ya manyoya hayo imara mle ndani. Mama akawachukua tu, bila mtetemo wa mbawa hizo, na kujinyanyua kwenye upepo huo. Akaenda moja kwa moja miambani, kuwaficha kutokana na dhoruba iliyokuwa inakuja.

159 Loo, ndugu, dhoruba iko karibu. Isikie Sauti Yake. Inakuita, "Ondoka Babeli. Ukajitenge. Usishiriki dhambi yake, zao. Nitawapokea. Mtakuwa wana na binti Zangu. Nitakuwa Mungu kwenu."

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu, katika kufunga. [Ndugu mmoja anatoa unabii—Mh.]

160 Amina. Mlisikia huo. Huo ndio tunaoita unabii kanisani.

161 Je, kunaweza kuwako na wengine hapa asubuhi ya leo, ambao ninajua wapo, ambao wangesema, "Bwana Mungu, unirehemu. Ingawa nimejiunga na kanisa, nimekiri, lakini si—sijui kutulia mbele Zako ni nini, na kuisikia Sauti Yako ikiniongoza na kunifundisha. Nisingejua la kufanya kama ungezungumza nami kwa Sauti inayosikika. Ningependa kukujua Wewe, ili uweze kusema nami na kuzielekeza njia zangu"? Je, mnaweza kuinua mikono yenu sasa hivi na kusema, "Mungu, uturehemu"? Bwana awabariki, kila mahali, mikono kila mahali. Endeleeni tu kuiinua. Hiyo ni sawa. "Bwana, unirehemu. Nakuhitaji sana." Je, kunaweza kuwako na wengine kabla tu ya kufunga? Mungu anaiona mikono yenu huko nyuma, mama, na ninyi nyote huko nyuma, na wanaosimama kwenye safu na kadhalika. Mungu anawaona, hata jukwaani, huku juu kote.

Naye Samweli akasema, "Eli, uliniita?"

Eli akasema, "Hapana, mwanangu, sikukuita."

162 Huyo si mimi niliyezungumza na moyo wako, rafiki. Huyo alikuwa ni Mungu. Jibu tu na useme, "Mtumishi wako anasikia. Na uniweke katika uangalizi Wako, leo, Mungu. Nijalie, tangu siku hii, niwe Wako kabisa."

163 Mungu wa Milele, mpenzi wa nafsi, Muumba wa vitu vyote, wakati ile Sauti ndogo tulivu ya Mungu iliyonena na Samweli, iliyonena na Sauli, iliyonena na Petro, iliyonena na Danieli, na nabii Isaya, na kote katika nyakati, imenena tena asubuhi ya leo maskanini. Labda mikono thelathini, au arobaini, au labda hamsini, ya wenye dhambi na washiriki wa kanisa, na watu waliovurugika, waliinua mikono yao. Wengi wao walikuwa hapa jana usiku, nao wakasikia Sauti Yako ikisikika. Na sasa, asubuhi ya leo, Sauti iyo hiyo inanena kwenye kilindi cha mioyo yao. Wameinua mikono yao, huku mikono yao imeelekezwa Mbinguni, wakisema kwamba wamekosea, na wanataka kuwa sahihi.

164 Umesema katika Neno Lako, kwamba, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote watakaokuja, nitawapa Uzima wa Milele. Nami nitamfufua katika siku ya mwisho."

165 Uliahidi hilo, Baba. Sasa tunakuomba Wewe, kama mtumishi Wako, kuwapa hawa walioinua mikono yao, Uzima wa Milele na furaha ya Milele. Na jalia wakuishie Wewe, siku zote za maisha yao. Na mwishoni mwa safari ya maisha, waingie katika furaha ya Bwana. Tujalie, Baba. Tunaomba katika Jina la Yesu na kwa ajili ya Yesu. Amina.

166 Ni wangapi wenu mnampenda kwa mioyo yenu yote, mioyo yenu yote? Sasa, katika sehemu hizi ndogo hapa namna hii . . . Nimechelewa tu. Lakini Biblia ilisema, ya kwamba, "Tunaketi pamoja katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu." Roho Mtakatifu anakuja, anaingia katika Neno, anashuka kupitia wasikilizaji, nawe unaweza kumtazama tu anapopitia juu yao, akiwabadilisha.

167 Kama nilivyosema, ninaamini katika mihemuko. Hakika. Lakini, wewe, nini . . . Unaona, mihemuko haikubadilishi. Mihemuko haina budi kuingia moja kwa moja mpaka iguse maadili ya nafsi yako. Hayo ndiyo yanayokubadilisha kutoka kwa ninii ya dhambi . . .

168 Mwenye dhambi ni nini? Asiyeamini. Kuna watu wengi siku hizi, wenye Sha—Shahada ya Sanaa, wenye shahada ya uzamifu, wenye Ph. D., na L. maradufu D. kwenye jina lao, na wangali ni wenye dhambi. Wanaijua Biblia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, wanahubiri mimbarani, na bado wanaami- . . . hawaamini. Biblia ilisema, "Asiyeamini amekwisha kuhukumiwa tayari."

169 Uliza mmoja wa hao watu kama wanaamini kwamba Roho Mtakatifu ni kwa ajili ya siku hizi. "Mbona, la, hasha." Je, unaamini ya kwamba uponyaji wa Kiungu upo? "Mbona, la, hasha." Basi yeye ni asiyeamini. Hiyo ni kweli. Ikiwa Roho Mtakatifu yuko ndani yako, je, hatashuhudia Neno Lake Mwenyewe? Na ikiwa roho aliye ndani yako anashuhudia kinyume na kile ambacho Mungu anasema ni kweli, huyo si Roho wa Kristo. Unaweza kuwa mfuasi wa church of Christ, lakini wewe si wa Kristo hadi roho yako iseme "amina" kwa kila ahadi aliyotoa Mungu. Na alipoahidi . . .

170 Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Basi kama roho yako inasema hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine . . . Maandiko yalisema nini? "Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu," Myahudi, "na watoto wenu, na kwa wale walio mbali," Mataifa, "hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Ahadi ile ile.

171 Yeye alisema, “Mimi ndimi Mzabibu, nanyi ni matawi.” Basi kama hilo ndilo Fundisho la tawi, tawi la kwanza, tawi la pili halina budi kuwa na Fundisho lile lile. Na Fundisho lile lile litatoa matokeo yale yale. Na kwa kuwa kila tawi linalokuja kwenye Mzabibu, litazaa kitu kile kile. Nina furaha, asubuhi ya leo, nina furaha sana kwamba najua kwamba Roho wa Mungu aliye hai angali anazungumza na kunena na watu, na kulithibitisha Neno Lake.

172 Tunaingia kwenye ibada ya ubatizo katika dakika chache tu. Ikiwa umenyunyiziwa, ukamwagiliwa, au kuzamishwa kwa njia yoyote ila katika Jina la Bwana Yesu Kristo, umepewa changamoto kuingia majini.

173 Sasa unasema, “Ndugu Branham, ungetaka kuniambia?” Ndiyo, ndugu.

174 Kunyunyizia hakujanenwa katika Biblia. Hakuna mahali katika Biblia ambapo mtu yeyote aliwahi kunyunyiziwa. Sasa kumbukeni hili. Nimeuliza dawati hili, juma zima. Nitafutieni ambapo mtu mmoja katika Biblia aliwahi kunyunyiziwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao, aliwahi kumwagiliwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao, au aliwahi kubatizwa kwa kuzamishwa katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu” kwa ondoleo la dhambi zao. Kamwe hapakuwapo na mtu aliyewahi kunyunyiziwa, kumwagiliwa ama kubatizwa kwa jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” katika vifuniko vyote vya Biblia. Hapana, bwana. Walikuwa . . .

175 Kulikuwako na watu waliobatizwa wakati mmoja na Yohana Mbatizaji, nao hawakubatizwa kwa jina lolote kamwe, nao walibatizwa na mtu yule yule aliyembatiza Yesu. Lakini Paulo, alipokutana nao katika Matendo 19, aliwaambia walipaswa kuja na kubatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo, la sivyo wasingeweza kumpokea Roho Mtakatifu bado.

176 Petro alipokutana na wengine waliompokea Roho Mtakatifu kabla hawajabatizwa hata kidogo, aliwaamuru na kukaa nao mpaka walipobatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Hiyo ni kweli, rafiki.

177 Najua watu wengi wanasema, “Sasa, Ndugu Branham ni Jesus Only.” Hilo si kweli.

178 Ninaamini tu Maandiko. Mimi si mfuasi wa madhehebu yoyote. Nao Jesus Only hawabatizi kwa njia hiyo, kwa vyovyote vile. Wanabatiza tu, Jina la “Yesu.” Biblia ilisema, “Bwana Yesu Kristo.” Kuna Yesu wengi, lakini Bwana Yesu Kristo mmoja tu. Mnaona? Mnaona? Kristo ndiye Masihi. Mnaona? Na hiyo ni kweli.

179 Na sasa, marafiki, sasa, ninyi mlio hapa asubuhi ya leo, hamjapata kubatizwa hivyo, Sauti ndogo tulivu ya Mungu na inene ndani kabisa ya nafsi yako. Na bila kujali yale askofu,

yale kanisa, yale kitu kingine chochote kinayosema, njoo ukamtii Bwana, ndiyo amri yangu kwako.

180 Na, sasa, Ndugu Neville atakwenda kwenye chumba *hiki*, kwa ajili ya kujiandaa kwa ajili ya ibada ya ubatizo. Na wale ambao—ambao wanavitayarisha vitu, baadhi ya wazee wataenda pamoja nami. Nitakuwa pamoja nanyi humo ndani, katika dakika moja tu.

181 Lakini nataka wale wanaokuja sasa, tutakapoimba, "Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita." "Nitaambatana Naye. Haidhuru ni kanisa gani, nitaambatana Naye. Bila kujali kile mtu yeyote, nitaambatana Naye kote njiani." Hebu wa—wanaume waingie kwenye chumba *hiki*, na wanawake waingie kwenye chumba *hiki*, tunapoimba sasa. Ndipo tutaruhusiwa kuondoka, rasmi, katika dakika moja tu sasa. Vema. Sote kwa pamoja sasa.

Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita,

182 Sasa, wanaume waende *hapa*, wanawake *huku*.

. . . Mwokozi wangu . . .

Baadhi ya wanawake waingie *huku* pamoja na wanawake hawa, tafadhalini.

Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu . . .

Ulisikia nini? Sauti Yake.

"Jitwike msalaba Wangu, na unifuate, unifuate Mimi."

Popote Yeye . . . (Sasa kweli unalimaanisha?) . . . nitafuata,
Aniongozako nitafuata,
Aniongozako nitafuata,
Nitaambatana Naye, Naye kote njiani.

183 Sasa, ninaposema hivi, rafiki, nilisikia Sauti. Na kama hiyo Sauti haikunena kulingana na Sauti ya Mungu, *Hapa*, ni sauti ya uongo. Lakini, "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu."

184 Unawezaje kuja? Hii ndiyo sababu ya wewe kuja. Ni kwa sababu, "Jina lako liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Biblia ilisema hivyo. Wazia juu ya mtu ambaye ameketi na anajua kwamba hiyo ni Kweli ya Injili, na bado kitu fulani kinawashikilia, wakijua kwamba labda jina lao halikuwekwa. Nini basi?

"Wananiabudu bure." Tazama, "Bure."

185 "Loo," unasema, "Mimi ni mtu mwaminifu. Mimi ni mwaminifu . . . " Hilo halina uhusiano wowote nalo.

186 "Wananiabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu."

187 Nimewaambia, hakuna mtu aliyenyunyiziwa, akamwagiliwa, au kubatizwa, kwa jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu” katika Biblia. Patafute. Patafute. Kama papo, njoo unionyeshe, jukwaani usiku wa leo. Basi, ikiwa umefanywa hivyo, unafuata mapokeo ya wanadamu.

188 Na kama mtu atakwambia, “Vema, njoo ukafanye maungamo yako, utampokea Roho Mtakatifu basi.” Huo ni uongo. Hilo ni fundisho la kujibunia.

189 Kuna ubatizo wa uongo wa maji. Kuna ubatizo wa uongo wa Roho Mtakatifu. Ibilisi anauigiza kwa sababu yeye ni wa kidini. Kaini, baba yake alikuwa mtu wa dini, kama tulivyolipitia. Uzao wa nyoka ungali unaendelea. Na Uzao wa mwanamke, kupitia Kristo, ungali unaendelea.

“Lakini, hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu.”

190 Sasa wazia baadhi ya watu wanaoketi hapa, asubuhi ya leo, ambao mnajua kwamba mmebatizwa kwa njia isiyofaa, katika kanuni za imani ya mwanadamu, wala si kulingana na Biblia, na kuzaliwa kwako mara ya kwanza kwa maungamo ni makosa. Unawezaje kuwa sawa, isipokuwa urudi nyuma na kuanza vizuri? Mnakumbuka, juma hili, nimehubiri: *Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo*.

191 Sasa, na kama unaweza kusikia Sauti ikisema nawe, huyo ni Mungu, kwa maana inapatana na Maandiko. Ikiwa sivyo, basi kuna aina fulani ya sauti isiyo sahihi inayozungumza nawe. Lakini Sauti sahihi itakwambia ufuate kanuni za Biblia; hakuna kunyunyiziwa, hakuna kumwagiliwa, hakuna kwa njia isiyofaa. Njoo moja kwa moja na ufuate kanuni za Biblia.

192 Fanyeni hivyo, marafiki, kama itachukua kila kitu. Sijali ingegharimu nini, nitaweka kando kila kitu, kumfuata Bwana Yesu.

193 “Sikia Sauti Yangu. Kondoo Wangu wataisikia, nao watakuja Kwangu. Na wote watakaonijia Mimi, nitawapa Uzima wa milele, na kumfufua katika siku za mwisho.” Hiyo ni kweli?

194 Hili hapa, moja kwa moja pamoja na Maandiko. Hakuna anayeweza kukanusha Hilo. Hiyo ni kweli. Hakuna anayeweza kukanusha Hilo. Hili hapa, katika Nguvu za Roho, akifanya mambo yale yale ambayo Yesu alifanya. Huyu *hapa*, kwenye picha, Nguzo ile ile ya Moto, ikitembea, matunda yale yale, Roho yule yule, akiwa na mhemuko ule ule, tendo lile lile, ishara zile zile, maajabu yale yale. Haya basi. Isikie Sauti ya Mungu asubuhi ya leo.

Nayo ile Sauti ilisema, “Samweli.”

195 Kasema, “Naam, Bwana. Naam, Bwana. Mimi hapa. Huyu hapa mtumishi Wako. Huyu hapa mtumishi Wako. Nitafuata.”

Mungu ambariki mama huyo. “Nita . . . ”

196 Unasema, “Ndugu Branham, unasisitiza jambo hilo sana.” Nanakusudia kulisisitiza. Ni kati ya Uzima na mauti, kwa hivyo lazima nilikazie. Bwana awe nanyi, ndilo ombi langu aminifu.

197 Sasa, kabla hawajahamisha fenicha za jengo hapa, ili wapate. . .mpate kuona ubatizo. Mahali hapa ni wazi kila wakati. Ninataka kusoma baadhi yake, moja kwa moja kutoka kwenye Maandiko, ili mpate kuona ya kwamba ni—ninasoma.

198 Yesu Kristo, katika mlango wa 16 wa Mathayo Mtakatifu, ninaamini, alimwambia Petro, “Ninakupa funguo za Ufalme wa Mbinguni. Lolote utakalolifunga duniani, nitalifunga Mbinguni; chochote utakachofungua duniani, nitakifungua Mbinguni.” Nyote mnajua hivyo?

199 Kwenye siku ya Pentekoste, wakati Ufalme wa Mungu ulipokuwa umekuja katika utimilifu wa Nguvu Zake, je, mnaamini hilo? Petro, akisimama. Sasa, Yesu alipofufuka katika wafu, Yeye hakuwa na funguo za Ufalme. Hiyo ni kweli? [“Amina.”] Alikuwa na funguo za mauti na kuzimu, sio funguo za Ufalme. Na haya ndiyo aliyoyasema alipokuwa akihubiri, nao walikuwa wakisikia mambo haya, nao walikuwa wameifanya migumu mioyo yao. Haya hapa aliyosema Petro.

200 Sasa sikilizeni kwa makini ninaposoma Maandiko, mpate kuelewa. Matendo, mlango wa pili. Kumbukeni. Ni wangapi waliokuwa hapa kusikia yale mahubiri, *Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo*? Hebu turejee mwanzo tuone kile ubatizo, ubatizo ni nini hasa. Tunapaswa kubatizwaje? Kunyunyiziwa, kumwagiliwa, au kwa jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu”?

201 Kumbukeni, nimempa changamoto mhudumu yeyote, askofu yeyote, mtu yeyote, mahali popote, wakati wowote, anionyeshe Andiko moja ambapo mtu yeyote aliwahi kunyunyiziwa, kumwagiliwa, ama kubatizwa katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Ni wazi. Hauko katika Maandiko. Hapana.

202 Ni kanuni ya imani ya uongo, iliyobuniwa, iliyoanzishwa na kanisa Katoliki. Kunyunyiziwa kulianzishwa na kanisa Katoliki, karibu miaka mia sita baada ya kifo cha mwanafunzi wa mwisho. “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu” iliasiliwa wakati uo huo, kwa sababu Wakatoliki wanaabudu miungu mbalimbali, nao wakafanya utatu wa ofisi za Mungu. Si Miungu watatu; Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Huo ni upagani.

203 Kuna Mungu mmoja. “Usiwe na miungu mingine ila Mimi.” “Sikieni, enyi Israeli, Mimi ndimi Bwana, Mungu wenu, Mungu mmoja.”

204 Myahudi alituuliza, “Mungu wenu ni yupi; Baba, Mwana, au Roho Mtakatifu?”

205 Kuna Mmoja tu wao. Ni ofisi tatu ambazo Mungu yeye yule amefanya kazi ndani yake, akijidhihirisha Mwenyewe.

206 Kwanza, katika Baba, asingeweza kuguswa. Alining'inia mlimani; hata ng'ombe au mnyama angeugusa huo mlima, anapaswa auawe.

207 Ndipo akashuka, maana alitaka kuabudiwa. Akamkaribia mwanadamu zaidi, kwa maana alifanyika Mwana wa Adamu. Mungu alikuwa ndani Yake.

208 Basi alipofanya hivyo, ndipo akasema, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Hata hivyo, ninyi mtaniona, kwa maana Mimi," kiwakilishi nafsi, "nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Kasema, "Nalitoka kwa Mungu." Kitu gani? Nguzo ya Moto. "Narudi kwa Mungu." Alirudi? Alirudi. Ndipo basi alipofanya hivyo, akarudi kwa Mungu.

209 Ndipo tunamwona Paulo, katika somo letu asubuhi ya leo, akienda zake Dameski. Ndipo akakutana na Paulo njiani. Naye akambwaga chini. Ndipo Paulo alipotazama juu, Yeye alikuwa ni nini? Ile Nguzo ya Moto tena, Nuru iliyoyapofusha macho yake.

210 Angalia kile Yesu alichofanya alipokuwa duniani, na kumwambia yule mwanamke dhambi zake, akafanya mambo haya yote. Kisha akasema, "Sifanyi neno isipokuwa Baba anionyeshe kwanza."

211 Wakamwuliza, wakasema, "Kwa nini usishuke kwenda kule na kuwaponya hao watu huko chini?" Akapita katikati ya umati mkubwa wa watu, ambako viwete, vilema, vipofu na waliopooza. Akamponya mtu aliyekuwa na ugonjwa wa tezi dume, ama chochote kile, aliyelala kwenye godoro. Akasema, "Kwa nini usiwaponye kundi zima lao?"

212 Akasema, "Amin, amin . . ." Yohana Mtakatifu 5:19, sasa, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe; ila lile amwonalo Baba akilitenda, hilo atenda Mwana."

213 Huyu hapa amekuja tena, katika siku hizi za mwisho. Ulimwengu wa kisayansi hauwezi kulikanusha. Kanisa haliwezi kulikanusha. Hili hapa, limerudi moja kwa moja kanisani na kufanya jambo lile lile. Roho! Mungu anataka wale watakaoabudu katika Roho na katika Kweli. Huyu hapa.

214 Haya ndiyo aliyosema Siku ya Pentekoste, Petro akihubiri.

> *Huyu Yesu Mungu amemfufua*, wako wapi . . . sisi sote ni *mashahidi*. (Je, sisi ni mashahidi?)
>
> Kwa hiyo, *akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, . . . akiisha kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki, mnachokiona* ninyi *na kukisikia*.
>
> *Maana Daudi hakupanda* . . . mbinguni: bali *yeye mwenyewe* alisema, *Bwana alimwambia Bwana wangu, Keti upande wa mkono wangu wa kuume,*

> *Hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako.*
>
> *Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini, kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulibisha* ninyi *kuwa Bwana na Kristo.*
>
> *Basi waliposikia haya,* (hao walikuwa wale watu wa kidini) *waliposikia haya, walichomwa mioyo yao, nao wakamwambia Petro na...mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?*

215 Je, twende tu tuwe wema? La, la. Angalia, Petro, unazo funguo za Ufalme sasa. "Utakalowaambia," Mungu alisema, "Nitalifunga Mbinguni utakapolifunga duniani."

> *Petro akawaambia, Tubuni,* kila mmoja wenu mkabatizwe *kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*
>
> *Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa* wale walio *mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.*

216 Andiko moja zaidi. Miaka thelathini na miwili baada ya hayo, Paulo, hapa katika mlango wa 19.

> *Paulo, akiisha kupita kati ya nchi za juu,* akafika... *Efeso:* anakutana *na wanafunzi kadha wa kadha huko,*
>
> Naye *akawauliza, Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?*

217 Wabaptisti, acha hilo lizame ndani yenu. "Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?" Ni kuzaliwa, sio kukiri.

> *...Sisi hata* hatukujua *kwamba kuna Roho Mtakatifu.*
>
> *Akawauliza...Mlibatizwa...kwa ubatizo gani* basi? Walikuwa wamebatizwa, *Kwa ubatizo wa Yohana...*
>
> Paulo akawaambia, *Yohana kweli alibatiza...* kwa *toba*, (sio kwa ondoleo la dhambi), kwa *toba, akiwaambia...kwamba mnapaswa kumwamini yeye atakayekuja...yaani,* Yesu Kristo.
>
> Basi *waliposikia hayo, wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu* Kristo.
>
> ...na Paulo *akaweka mikono yake juu yao,* ndipo *Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakanena kwa lugha,* na kumtukuza Mungu.

218 Sasa acha niwapeleke, Paulo, akifunga waraka wake, Wagalatia 1:8.

> *...ijapokuwa sisi au malaika kutoka mbinguni, atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa* hiyo mliyokwisha kuisikia, *na* awe kwenu laana.

219 Ninaweza kuwapeleka pia kwenye Wakorintho, mlango wa 14, kifungu cha 38, ambapo ilisema.

> *Mtu yeyote* akikiri *kuwa ni* mtu wa *rohoni,* au nabii, *na ayatambue hayo*. . .yale *ninayowaandikia ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*
>
> *Lakini* mtu *akiwa mjinga, na awe* tu *mjinga.*

220 Tutafanya nini kuhusu hilo? Kila ushahidi . . . Mimi nilikuwa mahali pako, na sikuwa nimebatizwa kwa ubatizo wa Kikristo, bila kujali kanisa langu liliwazia nini, au mama yangu aliwazia nini, nataka kujua Bwana wangu anaagiza nini.

221 Bwana Yesu, ni Wako sasa. Nami naomba ya kwamba utafanya kazi katika kila moyo. Na uwape hawa, walio katika hili dimbwi kubatizwa, Roho Mtakatifu, wanapokungojea Wewe. Katika Jina la Yesu tunaukabidhi huu umati Kwako, ili kwamba kwenye Siku ile, Bwana, jalia nisiwe na hatia, bali niwe huru kutokana na damu ya watu wote; sio kusimama kwa mapokeo fulani, ama dhehebu fulani, ama shirika fulani, bali kwa kusimama kwa Neno Lako. Amina.

*Isikie Sauti Yake* SWA58-1005M
(Hear His Voice)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 5 Oktoba, 1958, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org